# Nipashe

Alhamisi Julai 9, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580279

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

HAKI YETU PROJECT

UNDER THE SAME SUN

215779502




## DC ajitoa mbio za ubunge, Nassari achukua kadi CCM

UKURASA 3

# Bashiru afunguka urais wa Zanzibar



Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally.

UKURASA 2

## BAA LA CORONA



### 'Usichukulie poa unategemewa'

* **Nawa mikono mara kwa mara kwa sabuni na maji tiririka**
* **Kaa kwa kuachiana nafasi hatua 2 au 3**
* **Vaa barakoa**
* **Ukikohoa au kupiga chafya ziba mdomo**




## MAKADA WAWILI CHADEMA WACHUKUA FOMU ZA URAIS

UKURASA 2

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Regnal Munisi (kulia), akikabidhi fomu ya kuwania kuteuliwa kugombea urais kwa Mwenyekiti wa chama hicho, Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



## NEC SASA YAANIKA WAANGALIZI UCHAGUZI

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu


**MICHEZO** **SIMBA HESHIMA, SHANGWE ZATAWALA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Makada zaidi CHADEMA wachukua fomu urais

**Na Mary Geofrey**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu, amekuwa mtia nia wa nne kuchukua fomu ya kuwania urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kwa tiketi ya chama hicho.

Wakati Nyalandu ambaye aliwahi kuwa Waziri katika serikali ya awamu ya nne akijitokeza, kada mwingine wa chama hicho, Wakili Gasper Mwanalyela, pia amejitosa katika kinyang'anyiro hicho.

Nyalandu amesema endapo atachaguliwa kupeperusha bendera kupitia chama hicho, aterejesha uhuru wa mihili ya Bunge, Mahakama na Utawala (Serikali) na kwamba anatamani Tanzania iliyo tofauti na ya sasa, isiyogawanyika na isiyo na fursa ya kuwagawanya Watanzania kimakundi.

Kauli hiyo aliitoa jana wakati akikabidhiwa fomu hiyo na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa CHADEMA, Reginald Munisi, katika Makao Makuu ya chama hicho, jijini Dar es Salaam.

Alisema anatamani kuiona Tanzania inayoongozwa na Katiba mpya, itakayodadavua na kurekebisha mifumo iliyoanza kuyumba kutokana na baadhi ya watu walioanza kuichakachukua kutokana na udhaifu wa mifumo hiyo.

"Wakati naondoka CCM nilisema ili nchi iwe sawa sawa ni lazima Serikali, Mahakama na Bunge viwe huru. Haya mafiga matatu yanatakiwa yajitegemee na yajiendeshe pamoja. Tunataka nchi ambayo mwananchi akikosewa na serikali yake awe na uhuru wa kuipeleka mahakamani," alisema.

Nyalandu ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii katika Serikali ya Awamu ya Nne, alisema atarejesha umoja wa kitaifa na kuondoa tofauti za kisiasa.

"Jambo la kwanza ni kuhakikisha tunarejesha umoja wa kitaifa. Matumaini ya Watanzania ya udugu, upendano na ushirikiano, penye lawama tupeleke upendo. Nilipokuwa CCM nilimshika mkono (Freeman) Mbowe (Mwenyekiti wa CHADEMA) na tukafanya kazi. Umoja ule wa kitaifa upite tofauti zetu tunazoziona," alisema Nyalandu.

**WAKILI MWANALYELA**

Awali, Wakili wa Mahakama Kuu Tanzania, Mwanalyela, alikuwa mwanachama wa tatu kuchukua fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea urais wa Tanzania kupitia CHADEMA, huku akitanabahisha kuwa ameamua kugombea ili kurudisha matumaini kwa wananchi walio na hofu na wenye kukata tamaa. Pia alisema atafuata nyayo za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, za kuanzisha vijiji vya ujamaa na kujitegemea na kwamba, atakwenda mbali zaidi kwa kuanzisha vijiji vya wataalamu.

"Baba wa Taifa alianzisha vijiji vya ujamaa na kujitegemea. Tunapaswa kutengeza vijiji vya wataalamu wa madaktari, teknolojia na kilimo. Vijiji hivi ni muhimu kuongeza ugunduzi na uvumbuzi," alisema. Alisema endapo atateuliwa na CHADEMA kugombea urais na kisha kuchaguliwa na wananchi kuwa Rais wa Tanzania, atahakikisha Katiba ya wananchi inapatikana, pamoja na kutoa elimu ya uraia kwa wananchi ili wajue haki na majukumu yao katika Taifa. Pia alisema suala hilo litakwenda sambamba na upatikanaji Katiba ya wananchi, kwa sababu ndani ya Katiba, mkataba wa kijamii unapatikana na kwamba ataufumua mfumo wa ulinzi na usalama, elimu, biashara, kilimo, teknolojia ili sekta hizo ziendane na mabadiliko ya sasa.

Mwanasheria wa CHADEMA, Tundu Lissu, alikuwa wa kwanza kuchukua fomu Julai 4, kupitia wakala wake David Jumbe. Dk. Mayrose Majinge alikuwa wa pili kwa kuchukua fomu juzi.

Kuanzia Julai 22 mwaka huu, Kamati Kuu ya CHADEMA itapendekeza jina la mgombea urais na Julai 29 mwaka huu, mkutano mkuu wa CHADEMA utapitisha jina la mgombea wa urais wa Tanzania Bara.




Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally (ndani ya gari), akikagua gari maalum litakalotumika na kikundi cha Tanzania One Theatre (TOT), wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu baada ya kulipokea makao mkuu ya chama hicho, jijini Dodoma jana. Kulia ni Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Mabodi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bashiru afunguka urais Zanzibar

**Na Joseph Mwendapole**

KATIBU Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, ameeleza kinachoendelea kuhusu mchakato wa kumpata mgombea urais wa Zanzibar, huku akiijibu hoja ya wanaodai kwamba mgombea urais kwa tiketi ya chama hicho hupatikana mkoani Dodoma.

Dk. Bashiru amesema tayari majina matano kati ya 31 ya waliojitokeza kuomba kuteuliwa kuwania nafasi hiyo yameshapatikana kwa ajili ya mchujo wa vikao vinavyofuata lakini hayatawekwa wazi kwa umma.

Aliyasema hayo jana kwenye mahojiano ya moja kwa moja na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya vyombo vya habari vya Azam, Tido Mhando, kwenye kipindi cha 'Uchaguzi 2020' ambacho ni mfululizo wa vipindi vya uchaguzi.

Majina hayo, kwa mujibu wa Bashiru, yataendelea kuwa siri hadi vikao vya uamuzi vitakapoamua kuyaweka wazi kwa kuwa kanuni za uongozi kuanzia shina hadi taifa zinawaongoza kutotaja siri za vikao.

"Vikao vya ngazi za juu vitakapoamua kwamba hii taarifa itolewe itatolewa lakini kwa sasa itabaki kuwa siri kama kanuni zinavyotuongoza na wale wenye kawaida ya kutoa siri za chama huwa tunawawajibisha kwa sababu wanakwenda kinyume cha utaratibu tuliojiwekea," alisema.

Alisema mchakato wa kumpata mgombea urais wa Zanzibar huanzia kwa wagombea kuchukua fomu na kisha uteuzi kufanywa na vikao maalum vya Kamati Maalum ya NEC baadaye Kamati Kuu ya chama na kisha Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC).

Akizungumzia madai ya baadhi ya watu kuwa rais wa Zanzibar huchaguliwa Dodoma, Dk. Bashiru alisema wanaosema hivyo wanapotosha kwa sababu chama hakimchagui rais bali kinateua mtu atakayepeperusha bendera ya chama hicho.

"Mchakato wa uteuzi wa mgombea hauwezi kuwa mchakato wa uchaguzi, hivyo ni vitu tofauti. Nadhani mawazo hayo hayawezi kuwa ya wana CCM, hivyo sioni haja ya kuyajadili kwa sababu naamini hakuna mwana CCM mwenye mawazo kama hayo.

"Kila chama kikishateua mgombea wake na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ikampitisha kwamba anakidhi vigezo, anakwenda na wenzake wa vyama vingine kupigiwa kura na Wazanzibari na siyo raia wengine ambao si wazanzibari," alisema Dk. Bashiru.

Kuhusu kujitokeza kwa idadi kubwa ya wagombea nafasi ya urais Zanzibar, Dk. Bashiru alisema hiyo ni dalili njema kwamba kuna demokrasia ya kweli kwa ndani ya chama hicho ambayo inataka kila mwanachama awe na haki ya kuchagua na kuchaguliwa.

Alisema si ajabu kujitokeza kwa wagombea wengi wa urais Zanzibar kwa sababu uzoefu unaonyesha kuwa hali imekuwa hivyo hata marais upande wa Bara wanapomaliza muda wao, idadi ya wanaoonyesha nia imekuwa kubwa kila mwaka.

Dk. Bashiru alisema hakuwa na shida ya wingi wa wagombea waliojitokeza bali alitoa angalizo kwa wanaojitokeza kuzingatia taratibu, kanuni na utii kwa chama chao kwa kuwa sifa zao ndizo zinaweza kukiimarisha chama au kukidhoofisha.

Alisema CCM ina uhakika kwamba mgombea itakayemsimamisha atashinda kwa kishindo kwa sababu atakuwa mpya tofauti na vyama vingine ambavyo vitasimamisha wagombea wale wale ambao ni wazoefu wa kushindwa.

Maalim Seif (Sharif Hamad) hawezi kumshinda mgombea wa CCM Zanzibar kwani chama cha ACT Wazalendo kitakachompitisha hakina mtandao mpana wa wanachama huku akisema kuwa atawezaje kama alishindwa akiwa CUF chenye mtandao mkubwa.

Alisema ana uhakika chama hicho kitapata ushindi wa kishindo Zanzibar na Tanzania kutokana na maendeleo makubwa ambayo Dk. Mohamed Shein ameyafanya kwa upande wa Zanzibar na Bara kwa maendeleo ambayo Rais John Magufulia amefanya.

Akizungumzia madai ya Tume Huru ya Uchaguzi (NEC), Dk. Bashiru alisema linajadilika ingawa anaamini kwamba tume za sasa zinauwezo mkubwa wa kuendesha chaguzi hizo kwa ustadi mkubwa.

"Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) zina uwezo na uzoefu mkubwa sana wa kuendesha chaguzi huru na haki na mimi sitaki kuamini kabisa kwamba tume hizi hazina uwezo huo na nahimiza tulinde uimara wa tume zetu na kuondoa kasoro ndogo ndogo," alisema.

Kuhusu kama Bunge lijalo litafanya mabadiliko ili kumwongezea muda mwingine Rais John Magufuli baada ya mwaka 2025 , CCM italipokea jambo hilo kwa mikono miwili, alisisitiza kuwa Rais Magufuli hawezi kukubali mpango huo kwa kuwa atakwenda kinyume cha wosia wa Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere.

Alisema Rais Magufuli ametimiza ndoto za Mwalimu Nyerere kwa kukamilisha miradi mikubwa aliyokuwa akiipigania kama kuhamia Dodoma na ujenzi wa bwawa la umeme hivyo, hawezi kwenda kinyume naye.

HABARI KITAIFA

# DC ajitoa mbio kuwania ubunge, Nassari atua CCM

**Na Waandishi Wetu, ARUSHA**

MKUU wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amesema kwa sasa hana mpango wa kutangaza nia ya kuomba kuteuliwa kugombea ubunge katika majimbo ya Hai na Arusha Mjini ambako kwa muda mrefu alikuwa akitajwa.

"Mimi leo nimesimama hapa kutoa shukrani kwamba Mungu ametenda maajabu na mimi siwezi kuyaelezea. Ni heshima kusema kwamba hayo yalifanyika (kuteuliwa kuwa mkuu wa wilaya) nikiwa Diwani wa Sambasha na muda wangu umekoma.

"Watu wakikutajataja hata kama siyo wapigakura, wakasemasema, maana yake wanakuambia habari njema kuhusu wewe na niwaambie tu watu wa Sambasha inawezekana wametaja kuhusu Arusha hata hapa, hata huko Hai, lakini nimekuja kuwaambia sitagombea udiwani tena, wala sitagombea ubunge popote," alisema.

Ole Sabaya alisema kwake ni heshima kubwa zaidi, siyo tu kuteuliwa na Rais, lakini kuteuliwa na Rais aina ya Dk. John Magufuli, akikuelezea kuwa ni habari kubwa zaidi.

"Heshima hiyo niliyoitamka hapa, mtu aliyekunyanyua katika kipindi ambacho watu wengine wote hawakuamini na baadaye baadhi ya wale watu wakarudi wakasema unafanya kazi njema, walewale!

"Mimi huyo huyo niamke niende nikatafute nafasi nyingine, kwangu haitakuwa na thamani ya ubunge, ila nitakuwa nimetambulisha kama mtu mwenye uchu na tamaa," alisema.

Alisema ataendelea kuwatumikia wananchi wa Hai hadi hapo Mungu na Rais Magufuli atakapoamua vinginevyo.

Wakati Ole Sabaya akiweka msimamo huo, Mbunge wa zamani wa Arumeru Mashariki (CHADEMA), Joshua Nassari, amejiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM), akieleza kuvutiwa na juhudi za Rais Magufuli kubadili sura ya Tanzania kimataifa.

"Kweli ninakishukuru chama changu (CHADEMA) kwa kunilea na kunifikisha hapa nilipo, lakini roho yangu inakataa kuendelea kubaki huko na kupinga yanayofanywa na Rais wangu (Magufuli) kama mashamba ya Valeska na Madila na mengine ambayo niliyapigania turudishiwe toka mikononi mwa wawekezaji na Rais ameyarudisha na sasa ni ardhi ya wananchi wa Meru," Nassari alisema jana.

Nassari aliyekuwa ameongozana na Ole Sabaya na kupokewa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana CCM Taifa (UVCCM), Kheri James katika Ofisi za CCM Mkoa wa Arusha, alisema kama si Rais Magufuli, suala la Tanzania kutangazwa ulimwenguni kwa sasa kuingia katika orodha ya nchi zenye uchumi wa kati, ingekuwa ni ndoto.

"Sikuwahi kuwaza kama ipo siku nitatamka 'CCM oyee', lakini baada ya kutafakari kwa muda mrefu, roho yangu inakataa kabisa kubaki upinzani, Rais Magufuli ametekeleza yote niliyoyapigania ikiwamo kurudisha ardhi ya watu wa Meru ambayo nimeipigania miaka yote.

"Roho yangu imeniambia nijiunge na CCM, marafiki walionichangia, ndugu na jamaa wote wamenishauri jambo hili la kujiunga CCM mchana kweupe, kwa sababu ninaipenda nchi yangu na ninaondoka siyo bahati mbaya.

"Ninaomba radhi wale wote watakaokwazika kuniona nimerudi CCM, wanisamehe kwa sababu roho yangu imekataa kubaki upinzani wakati kuna mazuri mengi yanayofanywa na CCM kupitia Rais Magufuli na nimeshaandika barua ya kutaarifu chama changu cha zamani, kuhusu uamuzi huu na nimeambatanisha na kadi yao kuwarudishia," alisema.

■**Imeandikwa na Cynthia Mwilolezi na Godfrey Mushi**



Wananchi wakichukua tahadhari ya maambukizi ya ugonjwa wa corona kwa kunawa mikono kabla ya kuingia katika Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NEC yaanika asasi elimu ya mpigakura

**Na Salome Kitomari**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetangaza asasi 245 za kiraia zilizopewa vibali vya kutoa elimu ya mpigakura katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, huku asasi 97 zimepewa kibali cha kuwa waangalizi wa uchaguzi, huku saba zikiruhusiwa kutoa elimu ya mpigakura Visiwani Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa iliyopo kwenye tovuti ya NEC juzi na kutiwa saini na Mkurugenzi wa Uchaguzi, Dk. Wilson Charles, asasi hizo ziliwasilisha maombi Januari 20, mwaka huu.

"Baada ya uhakiki na kufanya upembuzi wa maombi yaliyopokelewa, taasisi/asasi saba zilikidhi vigezo na kustahili kupewa vibali kwa ajili ya kutoa elimu ya mpigakura kwa upande wa Tanzania Zanzibar," alisema.

Alizitaja asasi hizo kuwa ni Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA), Pemba Association for Society Organization, Shirikisho la Michezo ya Viziwi Zanzibar.

Zingine ni Tanzania Women Political Enhancement Network Zanzibar Zone (TWOPENZZ), Umoja wa Madereva na Utingo Zanzibar (UMUZA), Umoja wa Ujirani Mwema Zanzibar (UJIMWEZA) na Zanzibar Fighting Against Youth Challenges Org.

"Tume inazitaka asasi zote zilizopewa vibali kuzingatia taratibu na kanuni zinazoongoza suala hilo, ikiwamo mwongozo wa utoaji wa elimu ya mpigakura...Asasi zilizopewa vibali zitalazimika kushiriki semina maalum ya kupitia mwongozo huo," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, mwishoni wa mwezi uliopita, Tume ilibainisha kasoro katika asasi zilizoomba vibali ikiwamo kutosajiliwa kwenye masjala, kutokuwa na ofisi, kushindwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo, kuwasilisha maombi ya kutoa elimu ya uraia badala ya elimu ya mpigakura.

Kasoro zingine ni kuwasilisha maombi bila kueleza maeneo zinayotaka kutoa elimu, malengo ya asasi kutoendana na utoaji elimu, kutowasilisha nyaraka muhimu kama katiba, cheti cha usajili na ratiba, kutowasilisha ordha kamili ya majina ya watendaji wakuu na kutoonyesha njia za mawasiliano.


Kwa idhini tuliyopewa na **HARBOUR MICROFINANCE COMPANY LIMITED** Sisi **J.J. RECOVERY** tunatoa taarifa kwa mdaiwa kulipa deni unalodaiwa ndani ya siku 14 ya tangazo hili baada ya hapo tutauza gari lililo orodheshwa hapo chini.

| JINA | | AINA YA DHAMANA |
|---|---|---|
| 1. | LEVI IGNAS KADUMA | GARI, AINA YA BMW X1, RANGI YA SILVER YA MWAKA 2010, NAMBA YA USAJILI NI T 222 DCW. |

**Kwa mawasiliano wasiliana na:**
**J & J RECOVERY kwa namba 0714 292260 / 0784 076588.**



NORWEGIAN CHURCH AID
actalliance

## Advertisement on Business Opportunities

**INFORMATION ON BUSINESS OPPORTUNITIES**
**Date: 9th July 2020**
**Reference no: 02/NCA/2020**
**Subject: Provision of Consultancy Services**
**Contracting Authority: Norwegian Church Aid Tanzania**
**Deadline for submission of letter of interest: 15th July 2020**

**Background**
Norwegian Church Aid (NCA) is a Norwegian non-governmental and development organization working to promote Social Justice, Human Rights and Economic Justice for poor communities. NCA has its foundations based in the congregation of Churches in Norway, whose efforts are dedicated towards eradicating poverty, its causes and social deprivation. In Tanzania, NCA works in collaboration with local faith-based partners (FBOs)

Norwegian Church Aid Tanzania, in cooperation with its partner invites qualified individual consultants or firms in provision of the following services to respond to this advertisement.
Consultants who have responded to this advertisement and provide the required information will be shortlisted and the qualified ones will receive a Request for Proposal **(RFP)** for the relevant lot(s).

1. Capacity building on peace and interfaith relations
2. Agribusiness support/management
3. Gender based violence and SRHR issues
4. Research and evaluations
5. Training need assessment
6. Information and communications
7. Documentation of results
8. Business development
9. Design and manage online platform
10. Establishment and strengthening of AMCOS
11. Youth and Women Empowerment
12. Agribusiness development
13. Climate resilience or Climate Smart Agriculture or Climate change adaptation
14. Agricultural value chains and markets
15. Jobs and entrepreneurship for youths
16. Agricultural technologies (digital and non-digital)
17. Rural smallholder agriculture development
18. Baseline Study.
19. Impact assessment on Social Accountability Community Score Card Approach

The interested Consultants shall provide the following information to the Contracting Authority using the contact details below:
- Indicate which Consultancy service you are interested in.
- Provide the following information:
  - the individual or company's name and contact details;
  - contact person;
  - CV of individuals or brief description of the company's background and main line of work; and
  - experience with this kind of service.

**This is purely information on business opportunities and does not constitute a commitment to purchase or any other form of contractual commitment with the Contracting Authority.**
Due to the COVID-19 pandemic we are sorry that we are not accept hard copy of profiles, therefore all documents should be scanned in one original document in PDF format and send to Procurement.Tanzania@nca.no where the shortlisting will be done by the Procurement Committee and successful candidates will be contacted.

115803302

RIPOTI MAALUM -3

# Jumuiya Burunge hifadhi inayosimama kwa mtindo wa serikali, bajeti mabilioni

## ■Yabuni makusanyo utalii wa ndani
## ■Ilivyotikiswa miezi mitatu ya corona

**Na Salome Kitomari aliyekuwa** BABATI

UNAPOZUNGUMZIA Jumuiya ya Hifadhi za Jamii (WMA) Burunge, hapo unarejea kitu kikubwa zaidi mithili ya serikali, kwa maana ya kubeba vigezo vyote vya kiserikali, kuanzia muundo hadi matendo.

Lakini, waswahili wana msemo 'usione vyaelea vimeundwa'. Vivyo hivyo kwa Jumuiya ya Burunge, inayoteka mvuto wa umma kuanzia walio jirani na wa mbali kitaifa, ina historia yake.

Makamu Mwenyekiji wa WMA, Emmanuela Willium, anasimulia kwamba, Burunge ilianza kama eneo la majaribio mwaka 2003 na kanuni za kwanza za WMA zilitoka mwaka 2002.

Anasema kamati ndogo za maliasili za vijiji ziliunganishwa na kuunda WMA, kwa misingi ya kiikolojia na kupata kilomita za mraba 283 zilizofanyiwa usajili rasmi kisheria kuanzia Mei 2004.

Willium anasema makusanyo ya mapato, yalianza rasmi mwaka wa fedha 2006/07 kutoka maeneo ya uwekezaji. Hata hivyo, kutokana na dosari kadhaa, WMA ilianza kwa kusimamiwa na Halmashauri ya Babati, mahali iliko kuanzia mwaka 2012.

"Mwanzoni WMA ilipata asilimia 75 na 25 ilikwenda TAWA (Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania) na halmashauri. Mwaka 2006/07, zilipatikana Sh. milioni 37.4, nusu ilibaki na nyingine kwenda kwa vijiji wanachama," anafafanua.

Katibu wa Burunge, Benson Maise, anasema eneo hilo linaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori ya Mwaka 1998, ikipitia hatua kuanza kama eneo la majaribio kati ya mamlaka 16 za mwanzo zilizosajiliwa, yao ikiwa miongoni mwa nne zinazofanya vizuri.

"Kwa taratibu za uendeshaji, lazima kuwa na 'CBO' (asasi ndogo) ambayo inadhaminiwa na bodi ya wadhamini na kupata usajili kuwa na wawakilishi wa vijiji wanachama kwenye WMA, ambao wanapata kibali cha matumzi kilichopatikana mwaka 2017, kinachotoa uhalali wa kunufaika na wanyamapori," anaeleza.

Katibu huyo anasema walitumia mbinu ya kuunda kanda za matumizi katika vijiji 10 vilivyoko katika kata tatu. Anafafanua kwamba zipo kanda sita za matumizi kwa wakazi katika namna ya kwamba haziwanyimi kunufaika na rasilimali za wanyamapori.

Makamu Mwenyekiji Willium analifafanua hilo kwamba, wajumbe wa kamati maalum iliyoko (AA) wanatoka kila kijiji na kuunda Bunge linalojadili masuala mbalimbali kwa maendeleo endelevu.



Mwenyekiti wa Kijiji cha Olasiti, Daud Milengori akionyesha moja ya jengo la shule mpya ya msingi iliyojengwa kutokana na mapato ya WMA. **PICHA: SALOME KITOMARI**

**KANDA ZIKOJE?**

Kuhusu namna zilivyo, Willium ana ufafanuzi: "Kanda hizo ni za matumizi ya wageni ambako wanaruhusu kutengeneza huduma za utalii."

Anaendelea: "Kanda nyingine ni ushoroba (mapito ya wanyama) na kuna vitu vinakatazwa kufanyika, ili kuruhusu wanyama kupita kutoka Hifadhi ya Taifa Tarangire kwenda Ziwa Manyara."

Pia, katika muundo huo, anataja ukanda mwingine wa Ziwa Manyara na Burunge, ambazo kimuundo zinalenga kulinda matakwa ya vijiji vya wavuvi na kwamba ni maeneo muhimu kwa madini chumvi yanayotumiwa na wanyama kama nyumbu. Kimsingi, ndiyo eneo la kukuzia watoto kwa kuwa ni salama na kunapatikana majani laini wanayoyahitaji.

Mdau na mtaalamu huyo anaendelea na ufafanuzi kwamba, asilimia 98 ya Ziwa Burunge iko ndani ya WMA na pindi linapojaa maji, hudumu kwa kipindi cha miaka saba, hali iliyochukua sura mwaka huu.

Anasema pamoja na umuhimu huo, shughuli za uvuvi ndani ya ukanda huo nyeti kwa wanyama, hazijapigwa marufuku, ili kuendeleza kukidhi mahitaji ya binadamu, hapo ikigusa moja kwa moja utegemezi wa vijiji kama Vilima Vitatu, Ngolei, Mwada na Sangaiwe, ambako shughuli za umwagiliaji zimetawala.

"Tuna ukanda wa matumizi ya jumla ambao wananchi wanaruhusiwa kukata kuni, majani, nguzo, kulisha mifugo. Lakini, hufanyika kwa kufuata utaratibu wa kuomba kibali kwenye ofisi ya kijiji. Kubwa ni kuhakikisha haiathiri eneo la utalii," anafafanua katibu huyo.

Anataja ukanda mwingine ni wa uwindaji kitalii, ambao kampuni za uwindaji hupewa vibali ndani ya masharti kwamba wanahakikisha wanafanya kazi zao kwa kufuata sheria husika.

Pia kuna ukanda mwingine anaoutaja usioruhusiwa kwa matumizi yoyote, isipokuwa shughuli za kitafiti pekee na mahusus kwa wanafunzi wanaopatikana kando ya Hifadhi ya Taifa Tarangire.

**UWEKEZAJI NA MAPATO**

Willium anaorodhesha wawekezaji sita walionao, ambao ni Lake Burunge Tinted Lodge, Maramboi Tinted Lodge, Yulea, Tarangire River Camp, Tarangire Ospuko Lodge na wamiliki wa kitalu cha uwindaji, EBN Hunting Safari.

"Asilimia 75 ya mapato yote yanatokana na utalii wa picha. Mengine ni uwindaji wa kitalii na faini mbalimbali kwa wanaokwenda kinyume. Pia, tuna wahisani ambao wanaisaidia WMA kupitia huduma za kijamii na nyinginezo," anafafanua.

Kwa mujibu wa Makamu Mwenyekiti huyo, kasi ya ongezeko la mapato imekuwa juu kutoka Sh. milioni 37 mwaka 2006/07; mwaka 2007/08 (milioni 75.2); mwaka 2008/09 (Sh. milioni 64.5); mwaka 2009/2010 (Sh. milioni 391.4); mwaka 2010/11 (Sh. milioni 473.7); mwaka 2012/13 (Sh. milioni 275.4); na mwaka 2013/14 (Sh. milioni 412.5).

Vilevile, mwaka 2014/15 (Sh. milioni 820.94); mwaka 2015/16 (Sh. milioni 795.3); mwaka 2016/17 (Sh. bilioni 1.3); mwaka 2017/18 (Sh. bilioni 2.8); mwaka 2018/19 (Sh. bilioni 2.2); na mwaka 2019/20 (Sh. bilioni 2.5).

Anasema mwaka 2018/19 yalitokea mabadiliko ya kanuni ya kutoa mapato ya asilimia 75 kwenda TAWA asilimia 25 na halmashauri asilimia 10, na asilimia 65 inabaki WMA.

Makamu Mwenyekiti Willium anaeleza namna fedha hizo zinavyokusanywa na TAWA, kwa utaratibu wa mgeni wa Burunge kutakiwa kukata kibali katika ofisi maalum jijini Arusha.

Anaeleza namna wanavyowapokea wageni hao ni kwamba: "Tuna askari wetu kwenye kila lango ambao huhakiki vibali kabla ya mtalii kuingia. Kinachoangaliwa ni tarehe ya kuingia, kutoka na malipo aliyofanya na mwisho wa mwezi taarifa zinakusanywa na kupelekwa TAWA."

Makamu Mwenyekiti huyo anaeleza hatua za maboresho walizonazo hivi sasa, wameomba kutoka TAWA wawe na mfumo wa kukusanya mapato yao wenyewe, ili kuwa na uthabiti katika makusanyo yao.

"Tumeamua kuomba mfumo ili tuwe na utalii wa ndani, kwa kuwa kuna wananchi wanataka kutembelea hifadhi, lakini lazima waende Arusha kutafuta kibali, ndiyo waje waingie hifadhini jambo ambalo ni gharama mara mbili," anasema.

**PIGO LA CORONA**

Katibu wa Burunge Maise anasema mwaka wa 2019/20, walikadiria kukusanya Sh. bilioni 2.5, lakini kuanzia Mach 13 mwaka huu, hawajapokea mgeni yeyote kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. Anabainisha kuwa hadi kipindi hicho, walikuwa wamekusanya Sh. bilioni 1.4.

"Mgawanyo wa asilimia 65 nusu inabaki WMA kwa ajili ya uendeshaji na kwa mwaka huu, Sh. milioni 674.3 ambazo hulipa mishahara, kufanya matengenezo, kesi, mishahara, kodi za serikali na gharama nyinginezo, huku kiasi kama hicho kikienda kwenye vijiji.

"Mwaka 2018/19 tulikusanya Sh. bilioni 2.2 na kila kijiji kilipata Sh. milioni 100.9, lakini kutokana na janga la corona mgawo utakuwa Sh. milioni 67.5 kwa kila kijiji mwanachama," anasema.

"WMA tunakusanya na kuingiza katika misingi ya uendeshaji, hadi sasa kila kijiji kimeshapata Sh. milioni 446.7 kutoka mwaka 2006 hadi 2019, na zote zimefanya shughuli za maendelea na vijiji vyetu vina ofisi nzuri tofauti na vijiji vinavyotegemea michango ya wananchi."

**ITAENDELEA KESHO**

HABARI KITAIFA

## Mfumuko wa bei wabaki pale pale

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUMUKO wa bei wa Taifa, kwa mwaka ulioishia mwezi Juni, 2020 umebaki kuwa asilimia 3.2 kama ilivyokuwa kwa mwaka unaoishia mwezi Mei, 2020.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Sensa na Takwimu za Jamii wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ruth Minja, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Minja, alisema kutokana na hali hiyo, inamaanisha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia Juni, 2020 imebaki kuwa sawa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia Mei, 2020.

"Mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Juni, 2020 kuwa sawa na mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Mei 2020 kumechangiwa na kuongezeka na kupungua kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na bidhaa zisizo za vyakula kwa kipindi kilichoishia mwezi Juni, 2020 zikilinganishwa na bei za mwezi Juni, 2019," alifafanua Minja

Pia, alisema baadhi ya bidhaa za vyakula zilizopungua bei kwa Juni, 2020 zikilinganishwa na bei za Juni, 2019 ni pamoja na unga wa mahindi kwa asilimia 1.6, matunda kwa asilimia 2.1,viazi mviringo kwa asilimia 5.0 na mihogo kwa asilimia 13.3.

"Kwa upande mwingine, baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizoongezeka bei kwa Juni ,2020 zikilinganishwa na bei za Juni 2019 ni pamoja na mavazi kwa asilimia 2.7,gesi ya kupikia kwa asilimia 7.8, mkaa kwa asilimia 11.2, samaki kwa asilimia 2.7 na vitabu vya shule kwa asilimia 1.5,'" alisema Minja.

Vile vile, alisema mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia Juni,2020 umepungua hadi asilimia 3.8 kutoka asilimia 4.4 kwa mwaka ulioishia mwezi Mei,2020.

# Kampeni 'Nyumba ni Choo' yazindua mashine kunawia

**Na Somoe Ng'itu,** RUANGWA

MASHINE maalumu inayotoa majisafi yanayotiririka imezinduliwa rasmi kwenye Uwanja wa Majaliwa, ulioko katika Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi wilayani ikiwa ni mwendelezo maalumu wa kupambana na virusi vya ugonjwa wa corona (Covid 19).

Uzinduzi huo umefanyika jana kwa mashabiki waliongia uwanjani hapo kushuhudia mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya wenyeji Namungo FC dhidi ya mabingwa, Simba kutoka jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja Uhusiano wa kampeni ya Nyumba ni Choo, iliyoko chini ya Kampuni ya Project Clear, Kemilembe Mutahaba, alisema wamefanya uzinduzi huo ili kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kunawa mikono kwa maji yanayotiririka na sabuni. Alisema kaulimbiu ya mchakato huo ni 'Usichukulie Poa, Unategemewa' na hii inalenga kuikumbusha jamii kufikiria kulinda afya zao kwa sababu ya wategemezi wanaowahitaji katika familia zao.

"Kila mtu anategemewa, ana mtu anayemjali, kuna watoto, wazazi, mume au mke, hii inatufanya tuelewe kujilinda sawa sawa na maisha lazima yaendelee hata kama kuna corona," alisema Mutahaba.

Alisema Lindi ni mkoa wa pili kuzindua mradi huo baada ya kufanya hivyo jijini Dar es Salaam na wanatarajia pia kuzindua kwenye mikoa mingine 16.

Aliitaja mikoa itakayofuata ni pamoja na Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga, Mbeya, Iringa, Dodoma, Singida, Tanga, Mtwara, Kilimanjaro, Morogoro na Pwani.

Alisema mradi huo uko chini ya Wizara ya Afya na Nyumba ni Choo wameingia makubaliano na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), katika kutekeleza mpango huo kwenye viwanja vyote vinavyochezewa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha (kushoto), akimkabidhi cheti Mkuu wa Mauzo wa Vodacom, Kanda ya Kati, Grace Chambua, ikiwa ni kutambua mchango uliotolewa na kampuni hiyo kwenye Mashindano ya Kitaifa ya Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU 2020), yaliyofanyika mwaka huu jijini Dodoma jana. Vodacom imewazawadia Sh. milioni 20 washindi kutoka shule za msingi na sekondari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kigogo Halotel amwomba DPP yaishe

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imeambiwa kwamba Mkurugenzi wa Halotel, Son Nguyen (46) na vigogo wengine watano wa Kampuni ya Viettel Tanzania, wameandika barua kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), kwa ajili ya kukiri makosa yao 10.

Miongoni mwa makosa hayo ni la kuisababishia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) hasara zaidi ya Sh. bilioni 75.

Kesi hiyo ilipangwa kutajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Wakili wa utetezi Benedict Ishabakaki, alidai washtakiwa wamemwandikia DPP barua ya kuomba kukiri mashtaka yao.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa, na kwamba upelelezi wake bado haujakamilika, aliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Wakili Ishabakaki, alidai wateja wake walishaandika barua kwa DPP, na kuwa wanaendelea na mazungumzo.

"Mheshimiwa Hakimu, washtakiwa wameandika barua kwenda ofisi ya DPP kwa ajili ya kukiri makosa yao, ambapo wanaendelea na mazungumzo, hivyo tunaomba tarehe fupi," alidai Ishabakaki.

Akijibu hoja hizo, Wakili Wankyo, alidai kwa kuwa wanaendelea na mazungumzo, ni wajibu wa wakili wa utetezi kufuatilia mazungumzo hayo yalikofikia na yakiwa tayari wataiambia Mahakama.

Hakimu Simba, baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, alisema mazungumzo yakikamilika kabla ya siku ambayo watapangiwa kuletwa itatolewa hati ya kuletwa washtakiwa hao mahakamani.

Kesi iliahirishwa hadi Julai 22, mwaka huu kwa kutajwa na washtakiwa walirudishwa rumande.

Mbali na Nguyen, washtakiwa wengine ni Nguyen Minh (40) na Vu Tiep, wote ni Mameneja wa Halotel, Ha Than (39) ambaye Mtaalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Halotel, Mkurugenzi wa Fedha wa Kampuni hiyo, Nguyen Cong na Kampuni ya Viattel.

Wanadaiwa kutenda kosa kati ya Juni 8, mwaka 2017 na Machi 26, mwaka huu maeneo ya Mikocheni wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam, ambapo waliongoza genge la uhalifu ili kujipatia faida.

Ilidaiwa kati ya Juni 8, mwaka 2017 na Machi 26, mwaka huu maeneo ya Mikocheni, Dar es Salaam na maeneo mengine ya nchi kwa pamoja walitumia masafa ya redio bila kupata kibali kutoka TCRA.

Pia alidai kati ya Julai 7, mwaka 2016 na Machi 26, mwaka huu maeneo hayo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Vietnam kwa pamoja walitengeneza mfumo ambao ulitumia huduma za mawasiliano zinazojulikana kama Virtual Private Network (VPN) kinyume na taratibu.

Katika shtaka la nne, inadaiwa washtakiwa hao walikwepa kulipa kodi kwa TCRA kwa kutumia mitambo ya mawasiliano yaliyounganisha Viettel Tanzania na Vietnam kinyume na sheria.

Vile vile Juni 8, mwaka 2017 na Machi 26, mwaka huu maeneo hayo kwa kutumia masafa ya redio bila kupata kibali cha TCRA walisababishia mamlaka hiyo hasara ya Sh. bilioni 75.

Pia wanadaiwa kati ya Julai 7, mwaka 2016 na Machi 26, mwaka huu kwa kutumia mitambo ya VPN waliisababishia TCRA hasara ya Sh. bilioni 3.03.

Katika mashtaka saba washtakiwa wote wanadaiwa kutakatisha Sh. bilioni 3.03 wakati wakijua fedha hizo ni zao la makosa ya kuongoza genge la uhalifu.

Kampuni ya Viettel Tanzania inadaiwa kati ya Julai 7, mwaka 2016 na Machi 26, mwaka huu ilitakatisha Sh. bilioni 3.03 na mashtaka ya tisa na 10, washtakiwa wote wanadaiwa kutakatisha Sh. bilioni 75 wakati wakijua fedha hizo ni zao la uhalifu.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Maonyesho ya Sabasaba yachochee ukuaji viwanda

**MAONYESHO** ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayojulikana kama Sabasaba ambayo hufanyika kila mwaka, yana mchango mkubwa katika uchumi wa Tanzania.

Yana mchango huo kutokana na kutoa kuwakutanisha wafanyabiashara na kampuni za nchini na nje ya nchi, hivyo kutoa fursa za kufanyabiashara pamoja na fursa za uwekezaji.

Maonyesho hayo yalianza mwaka 1962 yakiwa ni kilimo yaliyokuwa yakifanyika katika viwanja vya Wizara ya Biashara na Ushirika kwa lengo la kukuza kilimo na ushirika.

Baadaye mwaka 1978 serikali iliunda Bodi ya Biashara ya Nje, ambayo ilipewa mamlaka kushughulikia usafirishaji wa bidhaa za kitanzania nje ya nchi. Bodi ya Biashara ya Nje ilipewa pia dhamana ya kukuza ushirikiano wa biashara ya kimataifa kupitia maonyesho ya kibiashara, kufanya utafiti kuhusiana na biashara.

Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni, maonyesho hayo yamekuwa yakishirikisha nchi takribani 20 za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) hivyo kama Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam na kufanyika kwenye viwanja vya Maonyesho vya Mwalimu Nyerere.

Kimsingi, lengo kuu la maonyesho hayo ni kuwakutanisha wafanyabiashara wakubwa, wajasiriamali pamoja na kampuni za nje, hivyo kuwa sehemu ya kuonyesha bidhaa mbalimbali wanazozizalisha zikiwamo za viwandani, kilimo, mifugo, utalii, uvuvi na za kazi za mikononi.

Maonyesho haya yamekuwa yakivutia wazalishaji wengi wa bidhaa kadri miaka inavyokwenda kiasi kwamba katika miaka ya karibuni maelfu ya kampuni zimekuwa zikishiriki kuonyesha bidhaa na huduma.

Ushiriki huo ni ishara kuwa maonyeshi haya yanatoa fursa kwa kampuni na wafanyabiashara binafsi kunufaika kwa njia mbalimbali zikiwamo za kupata maeneo ya uwekezaji pamoja na masoko ndani ya Tanzania na nje.

Ni jambo la kufurahisha kuwa maonyesho ya mwaka huu yaliyofunguliwa Julai 3 na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa yanashirikisha takribani jumla ya kampuni 3,000 kutoka nje na ndani ya Tanzania.

Tunasema hivyo kwa sasabu wakati huu ambao nchi yetu imepania kwa dhati kuwa ya viwanda, hivyo mchakato huo unahitaji uwekezaji zaidi katika ujenzi na viwanda nchini.

Hatua ya Benki ya Dunia (WB) wiki iliyopita ya kuitangaza Tanzania kuwa imeingia katika uchumi wa kati (kwa maana ya kipato cha kati kwa raia wake), ina maana kuwa sasa tunakoelekea katika uchumi wa juu njia ya kupita ni ujenzi wa viwanda.

Pengine ndiyo maana katika maonyesho ya mwaka huu serikali imelipa suala hilo msisitizo kwa kuyapa kaulimbiu ya 'Uchumi wa Viwanda kwa ajira na biashara endelevu'.

Tunashauri maonyesho hayo yaendelee kupewa kipaumbele ili yaendelee kupaniki na kuongeza fursa kwa Watanzania kwa kutoa sapoti katika ujenzi wa viwanda, hichochea uzalishaji katika sekta zingine za uzalishaji sambamba na kutoa ajira kwa wananchi hususan vijana.

Ni jambo linalotia moyo kusikia kauli ya Majaliwa wakati wa kufungua maonyesho hayo kwamba serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki na wezeshi ili kuviwezesha viwanda vidogo sana, vidogo na vya kati kukua na kufanya kazi kwa tija zaidi.


Waziri Mkuu ambaye alifungua maonyesho hayo kwa niaba ya Rais John Magufuli, alisema ili nchi iweze kuwa na mafanikio makubwa, taasisi za kifedha hazinabudi kuweka mikakati ya kutoa huduma ya mikopo rafiki ili kuwezesha ukuaji wa viwanda kwa kuzingatia viwanda vidogo na vya kati.

Bado kuna nafasi kwa wajasiriamali, wafanyabiashara wetu kuendelea kujifunza katika maonyesho haya katika muda uliobakia kabla ya kufungwa rasmi mwishoni mwa wiki.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Na Sabato Kasika

# Muungwana Lazima Nilonge

## Fursa ndio hizo shambani, wenye taaluma kazi kwenu

**WAHITIMU** wa vyuo vya kilimo kote nchini, wamekuwa wakihimizwa kutumia fursa ya uhaba wa maofisa ugani ulioko nchini, kwa kwenda kutoa elimu kwa wakulima na kuanzisha mashamba ya mfano kwa wakulima.

Lengo la kufanya hivyo ni kufungua mashamba ya mfano na watoe huduma kwa wakulima, pia ikiwa sehemu ya kujiajiri, kwa vile hivi kwa sasa nchi imebadilika. Wapo wakulima wanaotafuta wataalamu wa kilimo.

Wakulima wanafanya hivyo ili waweze kupata huduma kwenye shughuli zao za kilimo na wapo tayari kulipia wataalamu. Ni bahati mbaya, kwamba wataalamu wa ugani hawapatikani kwa ajili ya kazi hiyo. Fursa hii inatajwa na Naibu Waziri Kilimo, Omari Mgumba, kwamba inapaswa kuchangamkiwa na vijana waliohitimu vyuo, ili waweze kujikwamua kiuchumi, badala ya kukaa kusubiri ajira za serikalini.

Ni kweli kilimo kimebadilika na kinahitaji ushauri wa watalaamu, hivyo kama kuna wakulima wanaohitaji ushauri wa wataalamu hao, basi ni vyema wakachangamkia fursa inayotokana na uchache wa maofisa ugani.

Si kutoa ushauri wa kitaalamu tu, bali vijana hao pia wanatakiwa kuwekeza kwenye uzalishaji wa mbegu bora za mazao, kwa vile kuna uhitaji mkubwa wa mbegu nchini.

Kwa maelezo hayo ya naibu waziri, ni wazi kwamba hakuna haja ya kuzunguka na vyeti katika ofisi mbalimbali wakitafuta ajira badala yake wachangamkie fursa hiyo ya kufuata wakulima vijijini.

Haina mjadala kuna vijana wengi wanapohitimu shule na vyuo, mawazo yao ni kuhamia mijini kutafuta ajira. Hilo linaweza kuwa sawa, lakini kuna haja ya kujiongeza zaidi kwa kubadili mwelekeo.

Ndiyo maana serikali imekuwa ikiwahimiza wahitimu kuchangamkia fursa mbalimbali, badala ya kubweteka wakisubiri ajira, kwa sababu wanaweza kujikwamua kiuchumi kwa njia nyingine tofauti na taaluma yao.

Hivyo, hao waliohitimu kutoka vyuo vya kilimo, rai yangu kwao wasiendelee kusubiri ajira kwa kukwepa kwenda vijijini. Waangalie fursa, ikiwamo ya kukodishwa kwa ajili ya utalaamu wao, kwenda kufunza mbinu bora za kilimo.

Inawezekana wasipate malipo makubwa, lakini bado kuna unafuu kuliko kukaa kusubiri ajira, wakati kuna kazi tosha za kuwawezesha kupiga hatua moja ya kusonga mbele, katika harakati za kujiletea maendeleo.

Naibu Waziri huyo, ametaja kuwapo jumla ya vijana milioni 16.1 nchini, sawa na asilimia 35 ya idadi ya watu wote. Utafiti wa Nguvu Kazi ya Taifa wa mwaka 2014, ulioonyesha asilimia 67.1 ndio nguvukazi yote ya Taifa na kiwango cha ukosefu ajira ulioko sasa ni asilimia 11.7.

Hali inapokuwa hivyo, vijana hawana budi kubadilisha mwelekeo kwa kuchangamkia fursa zinazowawezesha kuendesha maisha yao, ikiwamo kuungana na kukopa fedha katika benki na wakajitosa katika biashara.

Takwimu hizo zinaonyesha umuhimu wa nguvukazi ya vijana na sekta ya kilimo kwa maendeleo ya nchi, ambayo kimsingi, kilimo bado ni uti wa mgongo wa taifa.

Naibu Waziri Mgumba kwenye wito wake ndani ya kongamano la vijana wakulima mkoani Arusha, anasema vijana wote waliohitimu vyou mbalimbali na kukaa kusubiri ajira bila kuangalia njia nyingine ya kujiajiri, ni hatari kwao.

Wametakiwa waanze kufikiria kujiajiri kwa kuishi na kutumia fursa ya mkopo wa asilimia nne unaotolewa katika halmashauri kwa vijana, ili wawe chachu ya mabadiliko katika jamii kupatikana ajira.

Kufikiria kujiajiri kunaweza kuongeza ajira kwa vijana wengine, kwani kuna uwezekano mkubwa wa kupata mkopo na kuanzisha biashara, ambayo wakati mwingine inamlazimu mkopaji aajiri wafanyakazi.

Baadhi yao wamekuwa wakilalamika kwamba, taasisi za fedha zimekuwa zikiwanyima mikopo, Niseme tu, ni vyema wakawekewa mazingira rafiki yanayowawezesha kuipata bila usumbufu.

Ni hatua itakayokuwa msaada mkubwa kwao, wakiachana na mazoea ya kusubiri kuajiriwa na badala yake watajiajiri kwani ninaamini wapo ambao wangependa kuona wanaendesha biashara zao na kuitwa 'mabosi.'

HABARI KITAIFA

## Watangaza nia watolewa hofu

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WATANGAZA nia kugombea nafasi ya ubunge Jimbo la Shinyanga Mjini, wameondolewa hofu ya kutotangazwa endapo watashinda katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Ofisa Organaizesheni, Uchaguzi, na Mipango wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Serengeti inayoounganisha mikoa Simiyu, Mara na Shinyanga, Joseph Ndatala, alisema hayo jana wakati watiania watatu wakichukua fomu kugombea nafasi hiyo Shinyanga Mjini.

Alisema watu waliotangaza nia ya kugombea nafasi ya ubunge Shinyanga Mjini wamefikia 11, lakini mpaka sasa waliochukua fomu ni watano tu, huku mchakato huo ukitarajiwa kukoma kesho.

"Napenda kuwatoa hofu watia nia wote wanaogombea nafasi ya ubunge Shinyanga Mjini. Wajitokeze kwa wingi kuja kuchukukua fomu ya kuomba kuteuliwa rasmi na chama na wasiogope kutotangazwa endapo watashinda kwenye uchaguzi mkuu bali watatangazwa tu," alisema Ndatala.

"Natoa wito pia kwa wanawake wajitokeze kwa wingi kuomba kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu. Wasijione dhaifu bali wanaweza kuongoza na ni viongozi wazuri tena wana misimamo na ni waaminifu katika utendaji wao kazi," aliongeza.

Naye mtangaza nia wa nafasi hiyo Shinyanga Mjini, Samsoni Ng'wagi, alisema amechukua fomu kuomba ridhaa ya kuteuliwa na chama kugombea nafasi ya ubunge, huku akiahidi kutatua changamoto ya uhaba wa maji na kuboresha miundombinu ya elimu.

Kwa upande wake, Zena Ghulam ambaye amechukua fomu ya kugombea nafasi ya ubunge wa viti maalum mkoani Shinyanga, alisema endapo atashinda kiti hicho, atatatua changamoto ya ukosefu wa vyumba maalumu kwa ajili ya kujistiri hedhi wanafunzi shuleni na kupigania kuondoa kodi ya taulo za kike.

# MOI yaokoa mtoto aliyetupwa

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), imefanikiwa kuokoa maisha ya mtoto wa kike mwenye miezi miwili, ambaye alikuwa amejeruhiwa kichwani baada ya kutupwa na mama yake.

Mtoto huyo waliyempa jina la Precious Moi, alipokelewa MOI Juni 29, mwaka huu, akitokea Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), baada ya kuokotwa na wasamaria wema.

Ofisa Uhusiano wa MOI, Patrick Mvungi, aliiambia Nipashe jana kuwa, mtoto huyo aliokotwa maeneo ya Tegeta akiwa ametupwa.

"Alifikishwa MOI akitokea Muhimbili baada ya kupata majeraha maeneo ya kichwani na tulipompokea alikuwa na hali mbaya, alikuwa ameumia zaidi maeneo ya kichwani kiasi kwamba alikuwa hawezi kufumbua macho," alisema Mvungi.

Alisema walianza kufanya uchunguzi wa kina na kumpatia matibabu kuanzia siku hiyo hadi hali yake ilipotengamaa.

"Kwa sasa anaendelea vizuri, baada ya kumpatia tiba na lishe ya kutosha kwa kushirikiana na watoa huduma wetu wa MOI," alisema Mvungi.

Kadhalika, Mvungi alisema watumishi wa hospitali hiyo, waliguswa na historia ya mtoto huyo, wakachanga fedha kwa ajili ya kumnunulia mavazi na kumpatia huduma nyingine muhimu za mtoto. MOI pamoja na kumtibia kwa mfumo wa kundi la msamaha wa matibabu pia wanagharamia maziwa yake kwa kipindi chote akiwa hospitalini hapo.

"Mtoto huyu aliwagusa watumishi wa MOI walimnunulia nguo za kutosha, nepi na MOI tunamhudumia maziwa na matibabu baada ya hapo tutamkabidhi kwenye kituo cha kulea watoto yatima," alisema.

Kutokana na mtoto huyo kutokuwa na ndugu wa kumlea, Mvungi alisema waliamua kumpatia jina la Precious MOI na baada ya hali yake kuimarika vyema watampeleka kwenye kituo cha kulelea watoto yatima.

Wasamaria wema waliomwokoa mtoto huyo hawajafuatilia hali yake, ndiyo sababu MOI imeamua kumpeleka kituo cha kulelea yatima.




Mkuu wa Tume ya Umwagiliaji, Kanda ya Kilimanjaro, Mhandisi Said Ibrahimu (kulia), akizungumza na baadhi ya wakulima wa mpunga katika Skimu ya Mawala, Moshi Vijijini jana, kuhusu namna serikali inavyokusudia kuboresha uvunaji wa zao hilo kwa mashine za kisasa ili kuongeza mnyororo wa thamani. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Mwanri asifiwa kuigeuza Tabora ya kijani

**Na Welingtone Masele,**
TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, amewataka wananchi pamoja na watendaji wa serikali wa mkoa huo, kudumisha mshikamano na ushirikiano ili kuharakisha maendeleo ya mkoa na kutatua changamoto zilizopo.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya makabidhiano baina yake na mtangulizi wake Aggrey Mwanri, ambaye amestaafu, mkuu huyo mpya, alisema ili kuhakikisha Mkoa wa Tabora unaendelea, ushirikiano baina ya watendaji wa serikali pamoja na wananchi unahitajika.

Sengati alimpongeza mtangulizi wake kwa kujenga misingi mizuri ya ushirikiano na mshikamano baina ya viongozi na jamii hatua itakayosaidia kuchochea maendeleo kwa wananchi, mkoa na taifa kwa ujumla.

Alisema Mwanri amejenga msingi mzuri wa watu kuchapa kazi na kuahidi kuendeleza msingi huo kwa kusimamia haki na kuimarisha usalama wa wananchi wa mkoa huo.

Alisisitiza kuwa ushirikiano mkubwa unahitajika baina ya viongozi na wananchi ili kuchochea maendeleo ya mkoa huo ambao kijiografia ni mkubwa kuliko mikoa yote hapa nchini, huku ukiwa na fursa nyingi za kiuchumi.

"Naomba sana tuendeleze ushirikiano huu ili yale mazuri yote yaliyoanzishwa na mtangulizi wangu Aggrey Mwanri hadi Tabora ikaitwa Toronto, yaendelee kudumu kwa manufaa ya wananchi na tufanye makubwa zaidi," alisema.

Kwa upande wake Mwanri ambaye amedumu katika nafasi hiyo kwa miaka mitano, aliwashukuru wananchi, watumishi, viongozi wa serikali, viongozi wa dini na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa ushirikiano mkubwa waliompa.

Alisema, ushirikiano huo umesaidia mkoa huo kupata mafanikio makubwa na kupiga hatua kubwa kimaendeleo ikiwamo kutatua changamoto za wananchi na kumtaka Mkuu mpya Sengati kuendeleza juhudi hizo ili kuondoa changamoto zilizopo.

Wananchi na viongozi waliohudhuria hafla hiyo, walimpongeza Mwanri kwa kuhamasisha utunzaji mazingira mkoani humo ambayo walisema sasa Tabora inang'aa, imekuwa kijani tupu.

Walimpongeza kwa kusimamia ipasavyo miradi ya maendeleo na kuhamasisha shughuli za kiuchumi ikiwamo kilimo cha tumbaku, pamba, alizeti, kuhamasisha elimu na kupiga vita mimba za utotoni.

# Serikali kufufua vyuo utafiti kilimo

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali itahakikisha vyuo na vituo vyote vya utafiti wa kilimo nchini vinafufuliwa, hivyo kuiagiza Wizara ya Kilimo kutenga fedha za kutosha katika bajeti yake kila mwaka.

Alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Naliendele iliyoko mkoani Mtwara kwa lengo la kujionea shughuli za utafiti wa mazao mbalimbali ya kilimo zinazoendelea kituoni hapo. "Nataka niwahakikishie serikali imedhamiria kuimarisha kilimo pamoja na utafiti wake. Mwezi mmoja uliopita nilikuwa Mlingano mkoani Tanga kuona shughuli za utafiti wa zao la mkonge, lakini miezi miwili iliyopita nilikuwa kwenye chuo kipya tulichokianzisha kule Kigoma cha Utafiti cha Kihinga na nimeona kazi yake na tutapata mafanikio makubwa," alisema.

Alisema Rais John Magufuli amefurahishwa na kazi nzuri za utafiti wa mazao zinazofanywa na vituo vya utafiti na matokeo mazuri ya utafiti huo kwa wakulima. "Azma ya kusimamia na kuona vyuo vya utafiti vinafanya kazi vizuri ni pamoja na maboresho haya. Kwanza wizara husika lazima itambue kuwa vyuo vya utafiti vina mchango mkubwa na wizara kwenye bajeti zake ipeleke fedha nyingi kwenye utafiti na tuone utafiti unagundua mambo na yale yanayogunduliwa yaende yakafanyiwe kazi," aliongeza.

Alisema udahili wa wanafunzi katika vyuo vya kilimo utaongezwa ili wapatikane wataalamu na watafiti wengi ambao wanahitajika katika kufanikisha mapinduzi ya kilimo nchini.

# Kampuni 94 za wabunifu zaanzishwa

Na Augusta Njoji, DODOMA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wiliam Ole Nasha, amesema kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), kampuni 94 zimeanzishwa na wabunifu wachanga kwa ajili ya kutatua kero mbalimbali za jamii na kujipatia kipato.

Pia amesema serikali imeendelea kuwaendeleza wabunifu mbalimbali ili ubunifu wao uwasaidie kujipatia kipato na kwamba katika kufanya hivyo, Sh. milioni 874 zimetengwa.

Ole Nasha alisema hayo jana alipokuwa akikabidhi zawadi kwa washindi 21 wa Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) kwa mwaka 2020 ambayo yamedhaminiwa na wadau mbalimbali ikiwemo Benki ya CRDB na kampuni ya simu za mkononi ya Vodacom Tanzania.

Alisema kuanzishwa kwa kampuni hizo kumezalisha ajira za moja kwa moja takribani 600 na kuwataka wabunifu kuendelea kubuni vitu na teknolojia zitakazosaidia jamii na kwamba kampuni hizo zimetoa ajira zisizo za moja kwa moja 15,000.

"Kwa 2018/19 teknolojia 231 na wabunifu 415 walitambuliwa na kati yao 60 waliendelezwa. Serikali kupitia COSTECH imeweka mazingira wezeshi ya kusaidia wabunifu wachanga," alisema.

Alisema kupitia tume hiyo utaratibu wa kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu wachanga kwa kuanzisha kundi la atamizi za ubunifu mpya 17.

"Endeleeni kuongeza kasi ya kuwatambua wabunifu nchi nzima na msisubiri wawafuate. Lengo letu ni ubunifu wao ufikie katika kiwango cha bidhaa ambazo zitaingia sokoni na kutumika na walaji (watumiaji)," alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, alisema mashindano hayo ni mkakati wa serikali kuibua na kuendeleza teknolojia zilizoanzishwa na vijana wa Kitanzania.

# BoT yaipa neno Benki ya NCBA

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Bernard Kibesse, ameitaka Benki ya NCBA kuibua fursa mpya katika nyanja zote za kiuchumi ikiwamo sekta ya kilimo na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Dk. Kibesse aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa huduma za benki ya NCBA ikiwa ni muunganiko kwa benki mbili ambazo ni NIC na CBA.

Alisema kwa niaba ya Gavana, wanaipongeza NCBA kwa uwazi walioуonyesha katika kufuata na kutimiza masharti na vigezo vya kisheria na kifedha hadi kufanikisha kuungana.

"Nimatarajio yetu mtaendesha shughuli zenu kwa uadilifu, uwazi na usawa kwa kufuata sheria, vigezo, masharti na viwango vya bora vya biashara vya kimataifa, mtakuwa mshiriki wa uhamasishaji kwa kusaidia wafanyabiashara, wafanyakazi, watu binafsi na wakulima kufanikisha maono yao," alisema.

"Mmesema mna wateja wengi Afrika, kuungana kwa taasisi hizi mbili ambazo ni benki ya CBA na NIC pamoja na kuanza rasmi kutoa huduma Tanzania kama benki ya NCBA kunafanyika baada ya kupokea leseni kutoka BoT," alisema.

Mwenyekiti Mteule wa Benki ya NCBA Tanzania, Sharmapal Aggarwal, alisema wanahamasisha ukuaji kupitia uvumbuzi wa kidigitali ili kuwapa watu msukumo wa kufanya mambo pasipo kurudi nyuma.


FURSA KWA WAGOMBEA!!!

Gazeti la Nipashe linatoa fursa kwa wagombea wote wa vyama vya siasa kunadi sera zao kupitia kurasa zetu kwa gharama nafuu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

Wasiliana nasi
The Guardian Limited
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



HABARI KITAIFA




Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Dk. Bernard Kibesse (kushoto), akiwa na Mkurugenzi Mkuu Mtendaji mteule wa Benki ya NCBA, Margaret Karume (wa pili kulia), Mkurugenzi Mteule wa Wateja Wakubwa, Binafsi na Wafanyabiashara wadogo na wa kati wa NCBA, Gift Shoko na Mwenyekiti Mteule wa Bodi ya NCBA, Sharmapal Aggarwal, baada ya uzinduzi wa benki mpya ya NCBA, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yatambulisha mikopo kwa wajasiriamali isiyo ya dhamana

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NBC imetambulisha mikopo isiyo na dhamana kwa wajasiriamali wadogo na wa kati nchini, lengo ni kuwasaidia waweze kukua kibiashara.

Kadhalika, lengo ni kuunga mkono jitihada za serikali katika kufanikisha uchumi wa viwanda.

Akizungumza kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara wa benki hiyo, Elvis Ndunguru, alisema mikopo hiyo inawalenga wajasiriamali wenye zabuni za kampuni kubwa.

"NBC tumechukua hatua hii ili kuwasaidia wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kutambua kwamba kwa kuwawezesha ndio tutakuwa tunaisaidia pia serikali kufanikisha agenda yake ya uchumi wa viwanda," alisema.

Hatua ya benki hiyo inakuja huku tafiti zikionyesha wajasiriamali wadogo na wa kati wanashikilia asilimia 95 ya biashara zote nchini na ni moja ya sekta zinazokua kwa kasi zaidi kiuchumi, huku ikichangia asilimia 35 ya Pato la Taifa (GDP).

"Hivyo basi, NBC tumeona kuna umuhimu wa kukua sambamba na sekta hii ambapo tumekuwa tukifanya tafiti mbalimbali za kimasoko ili kutoa huduma sahihi za kifedha zinazozingatia mahitaji yao kuelekea mafanikio ya ukuaji wa kiuchumi," alisema.

Alisema benki hiyo ilitoa mafunzo sambamba na kutoa mikopo yenye thamani zaidi ya Sh. bilioni 80 kwa wajasiriamali takribani 3,000 katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita pekee, huku akibainisha kuwa benki hiyo inatarajia kutoa mikopo zaidi.

Alizitaja sekta ambazo zimenufaika na mikopo hiyo ni za biashara, makandarasi, mafuta na gesi, utalii na hoteli, usafirishaji, viwanda na kilimo.

Kwa mujibu wa Ndunguru, benki hiyo inafanya mikakati mbalimbali ikiwamo kuipitia upya sera yake ya mikopo kwa wajasiriamali sambamba na kuunda kamati mpya ya mikopo ya biashara ili kuleta usawa katika kufanya maamuzi.

"Zaidi NBC tunatarajia kuondoa sharti linalowataka wajasiriamali kuandaa taarifa za kifedha pale wanapoomba mikopo iliyo chini ya Sh. milioni 100," alisema na kuongeza:

"Lengo haswa ni kuurahisisha mchakato wa mikopo na nyaraka zinazohitajika kutoka kwa wajasiriamali ili kuufanya mfumo uwe rahisi zaidi hatimaye kurahisisha ukuaji wa uchumi."

Alisema benki inapanga kuelimisha na kukaribisha vilabu vya biashara kwenye hafla mbalimbali pamoja na maonyesho ya kibiashara ili kuwawezesha wajasiriamali hao kukutana na wenzao wakubwa na wawekezaji kutoka nje.

Aliongeza kuwa benki hiyo imeanzisha mpango wa wajasiriamali ikilenga kujiimarisha zaidi katika soko linalohusu sekta hiyo.

# Waziri aja juu utozaji wa umeme bei kubwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ametoa onyo kali kwa wazalishaji binafsi wa umeme, wanaowatoza wananchi gharama kubwa tofauti na bei elekezi ya serikali.

Akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Kahunda, wilayani Sengerema Mkoa wa Mwanza, waziri alisisitiza kuwa gharama stahiki ya umeme kwa wenye matumizi ya kawaida ni shilingi 100 tu kwa uniti moja.

Alisema wananchi wanapaswa kutozwa gharama inayofanana katika maeneo yote nchini kwani wote wana haki sawa.

"Bei hiyo ni kwa maeneo yote nchini vikiwamo visiwa na ni kwa umeme wa aina zote pasipo kujali ni wa TANESCO au kutoka kwa wazalishaji binafsi wanaotumia umeme jua na aina nyinginezo," alisisitiza waziri.

Aliwaagiza viongozi wa serikali husussan wakuu wa wilaya kote nchini kuwachukulia hatua wazalishaji binafsi wa umeme, watakaobainika kukiuka mwongozo wa serikali.

Alisema amekuwa akipokea malalamiko kutoka kwa wananchi hususani wanaoishi visiwani, kwamba wamekuwa wakitozwa gharama kubwa na wawekezaji binafsi wa umeme hali inayosababisha wengi wajisikie kama wakimbizi ndani ya nchi yao.

Waziri alisema serikali haitavumilia tabia za aina hiyo zinazoonyeshwa na baadhi ya wawekezaji binafsi wa umeme kwani imewaamini kutenda haki katika kuwafikishia umeme wananchi hao ambao hawajafikiwa na gridi ya Taifa.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Emmanuel Kipole, alipongeza hatua za makusudi ambazo serikali kupitia Wizara ya Nishati, imekuwa ikizichukua katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora ya umeme.

## Red Cross yapongeza ujasiri wa Magufuli

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Msalaba Mwekundu Tanzania (Red Cross) Mkoa wa Dar es Salaam, kimempongeza Rais John Magufuli kwa ujasiri aliouonyesha katika mapambano dhidi ya Covid-19.

Chama hicho kimesema katika muda wote wa mapambano ya virusi hivyo vya corona nchini, walishirikiana na serikali katika mapambano hayo na jumla ya watumishi wake 500 walitoa huduma katika mkoa wa Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Red Cross Mkoa wa Dar es Salaam, Dollar Kusenga, alisema kazi kubwa ya mapambano ya corona yalifanywa na Rais Magufuli.

Alisema wanamshukuru Rais Magufuli kwa kuwa makini katika kutatua changamoto hiyo zikiwamo hatua za kuchukua kulingana na mazingira ya Tanzania bila kuiga mataifa mengine.

"Siyo tu kuwa makini bali alionyesha ujasiri wa hali ya juu bila kuangalia mataifa mengine wanafanya nini wala wanasema nini. Alionyesha uzalendo wake kwa serikali kushirikiana na taasisi binafsi katika mapambano hayo na hatimaye tumeshinda," alisema Kusenge.

Alisema amekuwa kiongozi wa mfano wa kuigwa na kutatua changamoto hiyo na kuwa sehemu ya mfano wa kuigwa na mataifa mengine duniani.

## 'Teknolojia muhimu uzalishaji viwandani'

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, amesema uzalishaji viwandani unategemea zaidi teknolojia.

Amesema teknolojia hiyo inatakiwa kuzalishwa nchini ili iwe na faida kuliko teknolojia itakayotoka nje ya nchi.

Dk. Akwilapo aliyasema hayo juzi jiji Dar es Salaam katika viwanja vya Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mjadala wa Siku ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, iliyowakutanisha wabunifu, watafiti na sekta binafsi.

Alisema teknolojia ikizalishwa nje ya nchi itakua ghali na kusababisha isiendane na mazingira yaliyokuwa ndani ya nchi.

## Benki ya UBA sasa yaunganishwa GePG

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imeiunganisha Benki ya UBA kwenye mfumo wa malipo wa serikali wa kielektroniki (GePG) ili kuwasaidia Watanzania waweze kulipa kodi kwenda taasisi zaidi ya 600 kwa haraka zaidi.

Mkuu wa kitengo cha sekta ya umma wa benki hiyo, Dominick Timothy, alisema na kueleza kuwa kwa sasa watu wataweza kulipa kwa haraka malipo ya kodi na yasiyo ya kodi kupitia UBA.

Alisema benki hiyo imepata kibali cha kuwa moja kati ya benki nane nchini zinazofanya malipo ya kodi na yasiyo ya kodi kwenda kwa taasisi za serikali kupitia mfumo wa GePG.

Timothy alisema kuwa kuunganishwa kwa benki yake katika mfumo wa GePG ni moja wapo ya njia za taasisi hiyo ya fedha kuunga mkono juhudi za maendeleo zinazofanywa na serikali chini ya Rais John Magufuli.

"Kutokana na benki yetu kuunganishwa na mfumo wa GePG itaoanisha mfumo huu na njia zake za kidijitali za kibenki ambazo ni kupata huduma kwa njia ya simu, mtandao na zile za Leo Chatbot, USSD Magic Banking na Webcollect," alisema.

Alisema lengo la kuunganisha na njia hizo za kibenki ni ili kuwawezesha Watanzania kufanya malipo ya serikali popote pale walipo pasipo kulazimishwa kwenda katika tawi la benki.

## Jamii yatakiwa kulinda misitu

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, ametoa wito kwa jamii, kushirikiana na serikali katika kulinda na kuhifadhi misitu kwa ajili ya faida ya kizazi cha sasa na cha baadaye.

Dk. Nzuki alitoa wito huo alipotembelea banda la Wizara ya Maliasili na Utalii kujionea shughuli mbalimbali zinazoendelea katika Maonyesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam katika viwanja vya Julius Nyerere.

Alisema misitu ni sekta muhimu ambayo inategemewa katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, hivyo kuna haja ya kuendelea kuitunza na kuilinda.

Aliupongeza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa shughuli inazozifanya za kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi wa misitu, uendelezaji utalii ikologia na malikale.

Dk. Nzuki alisema amaridhishwa na namna TFS ilivyojipanga katika maonyesho hayo na kuiagiza kuendelea kuboresha zaidi ikiwamo kufanyia kazi mapendekezo wanayopewa.

# DC abaini madudu ujenzi hospitali wilaya

**Na Welingtone Masele,** TABORA

MKUU wa Wilaya ya Tabora, Komanya Kitwala, ametembelea mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo unaotekelezwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.5 na kubaini kasoro za kiufundi.

Akiwa katika mradi huo unaojengwa kwa mfumo wa 'force account' na makandarasi wa ndani eneo la Inala, Kata ya Mpera Manispaa ya Tabora, Kitwala alisikitishwa na mpangilio wa kazi usioridhisha ikiwamo baadhi ya maeneo kutojengwa vizuri. Kutokana na kasoro hizo, aliagiza kufumuliwa maeneo yote yaliyojengwa chini ya kiwango kuanzia kwenye msingi na kujengwa upya kwa gharama za makandarasi.

Mtaalamu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) mkoani hapa, Goodluck Sanga, aliyeambatana na Mkuu wa Wilaya, alibainisha wazi kuwa msingi wa mradi huo haujajengwa kwa ubora unaotakiwa, hivyo unatakiwa kujengwa upya.

Alisisitiza kuwa ramani ya mradi haijafuatwa ipasavyo kuanzia ujenzi wa msingi jambo ambalo litahatarisha uimara wa kuta za majengo na kuongeza kuwa hata ukubwa wa nondo zilizopo kwenye mchoro sizo zilizotumika.

Sanga alisema sifa ya mkandarasi mzuri ni kutafsiri kwa vitendo mchoro wa kazi anayoifanya na kuhakikisha kila kilichoainishwa katika ramani yake kinafanyiwa kazi kama kilivyo na si kufanya vinginevyo.

Fundi anayesimamia ujenzi wa mradi huo, Mashaka Silika, alimhakikishia Mkuu wa Wilaya kuwa atafanyia kazi ushauri waliopewa ikiwamo kurekebisha kasoro zilizoonekana.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika Zahanati ya Kisiwa cha Rukuba, Musoma Vijijini mkoani Mara juzi, ikiwa ni uboreshaji wa huduma za afya. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wajasiriamali waitwa kusajili bidhaa

**Na Joseph Mwendapole**

WAJASIRIAMALI kote nchini wametakiwa kujitokeza kwa wingi kusajili bidhaa zao na vipodozi katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na maeneo yao wanayozalishia bidhaa za vyakula na kabla ya muda wa miezi mitatu waliopewa kumalizika.

Wito huo ulitolewa jana na Ofisa Uhusiano Mkuu wa TBS, Rhoida Andusamile, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye Maonesho ya 44 ya Biashara ya Kimataifa Dar es Salaam, maarufu kama Sabasaba yanayoendelea kwenye Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Barabara ya Kilwa.

Alisema TBS imekuwa ikishiriki maonesho ya Sabasaba kwa lengo la kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ambao watembelea maonesho hayo ili waweze kujua utaratibu wa kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozizalisha na kwa walaji waweze kutambua bidhaa bora ni zipi na zisizo na kiwango ni zipi.

Kwa mujibu wa Andusamile, katika maonesho ya mwaka huu wamekuja na nguvu ya kuhamasisha wajasiriamali kuhakikisha wanasajili bidhaa zao, vipodozi pamoja na maeneo yao wanayozalishia bidhaa za vyakula.

Alifafanua kuwa mwaka jana, Sheria ya Fedha Namba 8 ya Mwaka 2019 iliipa TBS mamlaka ya kusajili bidhaa za chakula na vipodozi, jukumu ambalo awali lilikuwa linasimamiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA).

"Kwa hiyo tangu Julai Mosi mwaka jana tumekuwa tukifanya kazi hii ya kusajili maeneo ya uzalishaji, maeneo ya kuhifadhia vyakula na vipodozi na vile vile kuthibitisha ubora wa bidhaa kazi ambayo tulikuwa tukiifanya tangu awali," alisema Andusamile.

Alisema wanatumia fursa ya kushiriki kwao maonyesho ya Sabasaba kuwahamasisha zaidi wajasirimali kujitokeza kwa wingi kujisajili kwani bado wanasuasua.

"Na tumeshatoa tangazo hivi karibuni kuwataka wasajili hizo bidhaa za vyakula na vipodozi, lakini bado wengi wanajivuta," alisema.

Alisema wajasiriamali waje wasajili na sasa hivi wanaweza kujisajili kwa njia ya mtandao kama wamekwama basi wafike ofisi za TBS ili wapate msaada.

Aliongeza kwamba kwa sasa wametoa muda wa miezi mitatu ili waweze kufanya hivyo na iwapo muda huo utamalizika, shirika la viwango wataanza kuwatembelea katika maeneo yao ya biashara.

"Tukiona hawajatekeleza maagizo haya basi hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yao, tunawasihi sana huo muda wa miezi mitatu waliopewa unaisha mwezi huu wa Julai mwishoni hivyo kuanzia Agosti tutaanza kuwakagua," alisema•

ALHAMISI JULAI 9, 2020
AFYA NA MAZINGIRA





Ukurasa 12

**Mimba na ngono za wanafunzi zilivyo pasua kichwa Kwimba**



Ukurasa 13

Tabia zake, jinsi zinavyoingia na namna zinavyoondolewa

Ukurasa 14

**Mtaalamu Mifugo anyambua viboko, mizigo, kuwafungia kunavyowatesa**

AFYA

# Tanga ya 2 kitaifa dawa kulevya, yapewa kituo tiba cha mil. 780/-

**Na Yasmine Protace**

KATIKA kuhakikisha waathirika wa dawa za kulevya wanapatiwa matibabu na kupona, kunatakiwa kuwepo kituo kwa ajili ya kuhudumia waathirika hao.

Kuwapo kituo ni sehemu ya mafanikio yanayowawezesha waathirika kunufaika na matibabu na ushauri.

Hivi kâribuni, serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imeendelea kuboresha huduma nchini na tayari kuna Sh. milioni 780, zimeshatolewa kujenga kliniki ya huduma za waathirika wa dawa ya kulevya, mkoani Tanga.

Waziri wa Afya Mendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ametaka hayo kwenye uzinduzi wa kituo cha muda cha kutoa tiba ya waathirika wa dawa za kulevya, kilichopo katika Hospitali ya Rufani ya Bombo, ambayo ni ya mkoa, jinini Tanga.

“Kwa kushirikiana na wadau wetu wa maendeleo Mfuko wa Dunia na Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya, tumepata zaidi ya Sh. milioni 780 na tumezileta kwa ajili ya kujenga jengo la kutolea huduma,” anasema Waziri Ummy.

Pia, ni fursa aliyotumia kupongeza uongozi wa mkoa wa Tanga, kutokana na ubunifu iliyoufanya kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, hapo anawataja wadau mahsusi PEPFAR na Amref, tawi la Tanzania.

Anasema asasi hizo zimejenga kituo cha muda, kwa ajili



Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, James Kaji.



Mkuu wa Mkoa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

ya kutoa tiba kwa warahibu wa dawa ya kulevya, akisema ujenzi wa kituo umegharibu jumla ya Sh. milioni 20.

“Tumeona tunaweza kufanya huduma hizi kwa gharama nafuu. Nafurahi kuona kwamba zimetumika takribani Sh. milioni 20 kwa ajili ya kutengeneza kituo cha muda kwa huduma za kliniki katika Mkoa wa Tanga” anasema Waziri Ummy.

Anafafanua kwamba, ilikuwapo haja ya kuwa na kliniki katika mkoa wa Tanga, kutokana na uhalisia mkoa huo kuwa katika nafasi ya pili ya kuwa na waathirika wengi wa dawa ya kulevya, akifafanua: “Takwimu za mwaka 2016, zinaonyesha mkoa wa Tanga una watumiaji taribani 5,190 wa dawa za kulevya.”

Waziri anasema, hadi sasa kuna jumla ya kiliniki nane nchini zinatoa huduma, akiutaja mkoa Dar es Salaam, kliniki hizo zimeshaanzia katika hospitali za mikoa kushuka chini kwenye hospitali za halmashauri na nyinginezo.

Anazitaja kuwa ni Hospitali za Kigamboni, Mbagala, Tegeta na zahanati ya Magereza Segerea, pamoja na Hospitali ya Wilaya Bagamoyo, mkoa wa Pwani.

Takwimu za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inarejea Tanzania ina waathirika 8,071 wanaopatiwa huduma dhidi ya kuathirika na dawa za kulevya, kati yao 480 ni wanawake na 7,591 wanaume.

**KAMISHNA DAWA KULEVYA**

Kamishna (wakati huo alikuwa kaimu) Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, James Kaji, anasema wiki hii kuwa Tanzania inaungana na mataifa mengine kuadhimisha Siku ya Kupinga Dawa ya Kulevya,

Katika hilo anataja kaulimbinu ya mwaka huu ni ‘Tujenge uelewa sahihi kwa tatizo la dawa za kulevya, ili kuimarisha mapambano dhidi ya tatizo hilo.’

“Uzinduzi wa kituo hiki ni mwendelezo wa vituo vingine vinane vinavyotoa huduma nchini, Dar es Salaam vipo vitatu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufani Mwananyamala na Temeke.

“Mbeya - Hospitali ya Rufani ya Nyanda za Juu Kusini; Mwanza - Hospitlai ya Rufani ya Sekou Toure; Bagamoyo na Dodoma - Itega” anafafanua Kamishna Jenerali Kaji

**RC TANGA**

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela, anasema Tanga imo katika mikoa yenye idadi kubwa ya shughuli za usafirishaji wa dawa za kulevya, hali inayoifanya kuwa na watumiaji wengi na urahibu wa dawa hizo.

Aidha, Shigela anaiasa jamii kuepuka matumizi ya dawa za kulevya ana anawaomba kutoa taarifa kwa mamlaka kuhusu uwepo, usafirishaji na biashara ya dawa za kulevya.

“Kwa wale ambao wameathirika na dawa za kulevya katika jamii zetu, tuwaone ni kama sehemu ya ndugu zetu. Tusiwanyanyapae, tuwaelekeze na tuwalete kwenye matibabu na tunaamini watarudi kwenye hali ya kawaida” anasisitiza Shigela

AFYA

# Mimba na ngono za wanafunzi zilivyo pasua kichwa Kwimba

## • Minada inavyowanasa kirahisi



Mnada wa Nyambiti wilayani Kwimba, unaotajwa kuwa miongoni mwa vichocheo vya mimba za utotoni, **PICHA ZOTE: NEEMA MICHAEL.**

**Na Neema Emmanuel, KWIMBA**

LICHA ya serikali na mitandao ya kijamii kama vile kwenye asasi za makanisani na misikitini, hospitalini kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia, zikiwamo mimba na ndoa za utotoni, bado tatizo ni sugu katika jamii na havijakoma.

Wilayani hapa bado kumeshamiri katika mazingira ya minada, waendesha bodaboda umbali mrefu, malezi na ng'ombe kutajwa vichocheo vikubwa vya matukio hayo.

Mimba za umri mdogo, pia uzao unaobebwa na uozeshaji watoto ni hatua inayoangukia kikwazo kikubwa kwa ukuaji maendeleo ya wilaya hasa kifaya, hata kunakatisha ndoto za watoto wanaopewa ujauzito katika umri mdogo.

**WANAVYORUBUNIWA**

Ofisa Tarafa ya Ibindo, wilayani Kwimba, Jeremiah John, ameiambia Nipashe kuwa wanafunzi wengi wanarubuniwa na waendesha pikipiki -bodaboda, kwa kigezo cha kuwapatia usafiri, huku wazazi nao wakiwaozesha, ili kujipatia mbadala wa ng'ombe.

Anasema katika tarafa yake yenye kata tisa na vijiji 36, inakabiliwa na changamoto kubwa ya mimba za utotoni kutoka kwa wanafunzi, hali inayochochea utoro na wanafunzi kuacha masomo.

Lawama kuu wanaelekezewa wazazi kwa malezi yasiyojali elimu, John akifafanua: "Juzi(wiki kadhaa zimepita) hapa kuna taarifa ilikuja kuna binti alifaulu kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, lakini baba yake alikuwa ameshamuozesha. Tulifuatilia na kufanikiwa kumrejesha shuleni binti.

"Tunajitahidi sana kutoa elimu kupitia mikutano ya hadhara kuwaelimisha, kwani jamii tuliyo nayo bado haijaamini kumsomesha mwanamke. Ni faida kubwa, wengine hufikia hatua ya kumshawishi mtoto afanye vibaya shuleni, ili amuozeshe. Unakuta hata akipata mimba, mzazi hajali na wala hatoi taarifa."

> **Unakuta binti anakuja mnadani pasipo kuwa na fedha, anachagua nguo, anafanya makubaliano na muuzaji kuwa ataenda kuchukua nguo hizo jioni, wakati wa kufunga.**

John anasema, ni hali inayochochewa na wazazi wengi kuwageuza watoto mitaji ya kubadilishana na ng'ombe, hivyo wito wake ni kwa wazazi kuachana na utamaduni huo, wakijikita katika mbadala kuwasomesha watoto, wanaofuatilia mienendo yao na hawawaruhusu kwenda kwenye minada.

"Unakuta binti anakuja mnadani pasipo kuwa na fedha, anachagua nguo, anafanya makubaliano na muuzaji kuwa ataenda kuchukua nguo hizo jioni, wakati wa kufunga.

"Hapo wanafanya yao, ndipo anapatiwa nguo. Huo ndio mchezo uliopo, kuna mabinti watatu niliwakuta wakichagua nguo, nilipowaita wanionyeshe wana Sh. ngapi hawakuwa na chochote...inasikitisha sana," anasimulia.

**DC AELEZA**

Mkuu wa Wilaya ya Kwimba, Senyi Nganga, anatoa mfano uliopo kila siku ya Jumatano, imekuwa siku yenye changamoto kubwa kwao, kwani watoto wengi wanaichukulia kuwa fursa ya kutenda maovu, wanayoambulia mbadala wa mimba kutoka kwa wasiowajua.

Senyi anasema, hivi sasa wanajikita katika utoaji elimu ya kujitambua kwa wanajamii, kutowapeleka watoto wao katika maeneo hayo hatarishi yanayowaweka katika athari.

Pia, ana mtazamo mwingine wa haja ya wazazi na jamii, kuzingatia malezi bora kwa kuongea na vijana wao na wanajamii kuhusu elimu ya makuzi kwa watoto wao na kutowaoza, kwa manufa ya mbadala wa ng'ombe.



Mwendesha bodaboda akiwa kwenye kituo chake cha biashara.

**WANAONYOOSHEWA VIDOLE**

John Mussa na Hassan Ally, ni baadhi ya wafanyabiashara wa minada katika soko la Nyambiti, Kwimba, ambao katika mazungumzo na Nipashe, wanaunga mkono dai dhidi yao kwamba, vijana wengi wanaozunguka minada wana tabia hiyo dhidi ya mabinti.

Mussa anadai kuwa, mabinti hao ndio wanaowaletea vishawishi vinavyochangia kufanyika kwa mambo hayo, pia akiwaelekezea lawama wazazi wa mabinti hao wenye jukumu la kuwalinda, wanawapa uhuru uliopitiliza.

"Tabia za huku ni chafu sana. Wengine wanaanza vitendo hivyo wakiwa na umri mdogo wa miaka 13 anajua kila kitu, msichana akija kuchagua nguo. ukiongea naye anakuambia yeye ndiye analisha familia.

"Akifika nyumbani anaulizwa 'mboga iko wapi' na haulizwi 'kwa nini amechelewa,' kwa hiyo wanaume 'wakikaona katoto hako' anakachukua na kukapa hela ya mboga," anasema Ally.

Pia, Januari Marezu, dereva wa bodaboda anasema umbali wa safari zinazowakabili watoto na kupenda lifti, ni chanzo kikubwa kwao kuingia kwenye uhusiano, wakiamini watapata ahueni kuwahi masomoni na kupatiwa mahitaji, ambayo baadhi hawazipati makwao kwa mzazi.

"Kuna kijana mmoja nilikuwa nafanya naye kazi, nilipoona tabia zake siyo nzuri, nilimshauri hadi akaacha. Ni wachache wanaokubali ushauri wengine wanapuuza," anasema Januari.

**WAZAZI JE?**

Wazazi na walezi kwa upande wao, wamefunguka na kutoa maoni ya kuitaka jamii kudumisha sera ya ushirikiano, kwa kumtazama mtoto wa mwenza, ni sawa na wake na wakati huo huo, wazazi hao kufuatilia kwa karibu mienendo ya watoto wao.

Miongoni mwa wazazi waliozungumza na Nipashe, Happy Kazimoto na Maganga Misungwi, mtazamo wao kuhusu mzizi wa tatizo wanaelekeza kwa wazazi kutojali na kufuatilia mwenendo wa watoto wao.

Inaelezwa, baadhi yao watoto wanaangukia matatizo hayo, pasipo wazazi kufahamu kinachoendelea na hufikia wakati wanafunguka macho ya kinachojiri, pale athari za wazi kama vile mimba zinapoanza kujitokeza, wakishakuwa wamechelewa.

Happy anasema, kinachopaswa kutawala sasa ni wazazi waendelee kupewa elimu sahihi, ili wamudu kuwanusuru vijana wao na adha hizo, akiendelea na hoja.

"Mtu amchukulie mtoto wa mwenzie kama wa kwake, kutasaidia sasa. Mtu anafanya unyama, kwa kuwa mtoto siyo wake, lakini akimchukulia kama wake, haya matukio yatakuwa historia," anahitimisha Happy.

***• Soma kesho mkasa wa kifamilia, ndoa ya mwanafunzi kwa mvuto wa mahari kutenguliwa.***

AFYA

VIDONDA TUMBO

# Tabia zake, jinsi zinavyoingia na namna zinavyoondolewa

## • Sigara, pombe, viungo... tafakari!

**Na Jackson Paulo**



Wagonjwa tofauti wakilalama vidonda vya tumbo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

VIDONDA vya tumbo vina namna yake vinavyotokea kwenye ukuta wa ndani wa utumbo, wa chakula au sehemu ya mwanzo ya utumbo mwembamba ujulikanao kama 'duodenum.'

Zipo aina kuu mbili za vidonda vya tumbo; vinavyotokea ndani ya mfuko wa tumbo, yaani 'gastric ulcers', pili hutokea kwenye sehemu ya mwanzoni ya utumbo mwembamba inaitwa 'duodenal ulcers'.

**CHANZO CHAKE**

Katika utumbo, huwa unamwagwa tindikali kwa ajili ya kusaidia mmeng'enyo wa chakula. Kwa kawaida, tindikali huwa ni kali na isipodhibitiwa tumboni, inaweza kuleta madhara.

Mfuko wa tumbo wa binadamu una ukuta wa ndani, uliozungukwa na ute (mucus) unaosaidia kuzuia tindikali isiunguze au kuharibu sehemu hiyo.

Uzalishaji ute huo unapopungua, una kawaida ya kusababisha tuindikali ama kuunguza/kuharibu sehemu ya ukuta wa tumbo, hivyo kusababisha vidonda vya tumbo.

Kupungua ute husababishwa na mambo. Kuna maambukizi ya bakteria ajulikanaye kwa jina la 'helicobacter pylori' (H. pylori), matumizi ya kipindi kirefu ya dawa za kundi la 'Nsaids' kama vile aspirini na 'ibuprofen.'

Pia, mazingira ya kuwepo tindikali nyingi iliyopitiliza tumboni (hyperacidity) ni hali inayohusiana na urithi wa asili, msongo wa mawazo, uvutaji sigara na matumizi ya baadhi ya vyakula kama pilipili na viungo.

Lingine, linaelezwa kitaalamu ni kuwepo tabia zinazomuweka mtu katika hatari ya kupata vidonda vya tumbo, ikijumuisha uvutaji sigara, matumizi makubwa asteroids' (kama dawa za kutibu asthma), historia ya familia kuwa na mgonjwa wa vidonda vya tumbo na matumizi ya pombe kupita kiasi.

**DALILI ZAKE**

Dalili za vidonda vya tumbo, hutegemea na hali ya vidonda vilivyo. Kuu inayowapata wengi ni kuhisi maumivu kama ya kuwaka moto eneo kati ya kifua na tumbo.

Kuna maumivu ambayo mara nyingi huwa makali zaidi, wakati tumbo likiwa halina chakula na inadumu kwa dakika chache au saa kadhaa.

Dalili nyingine, ni pamoja na kupungua uzito, kichefuchefu na kutapika, kushindwa kula kutokana na maumivu, kuhisi kuwa na gesi tumboni, kucheua au kupanda kwa tindikali kwenye koromeo, pamoja na kiungulia.

**UGUNDUZI HOSPITALI**

Kugundua vidonda na matibabu yake hospitali hutegemea dalili na hali ya vidonda vilivyo. Daktari huchunguza, kwa msada wa vipimo na anafanya mapitio ya historia ya mgonjwa na dalili au dawa alizowahi kutumia awali.

Ili kugundua uwepo wa bakteria H. Pylori'damu, kinyesi au kipimo cha mgonjwa hutumika.

Vipimo vingine vinavyoweza kutumika ni kinachoitwa 'Barium X-ray" na 'endos copy'. Hicho cha pili, mpira huingizwa tumboni mwa mgonjwa kupitia kinywa.

Kingine 'endoscopic biopsy' hufanyika kwa namna ya sehemu ndogo ya ukuta wa tumbo huchukuliwa na kufanyiwa vipimo.

**MATIBABU**

Matibabu ya maradhi hayo yanatofautiana, kulingana na chanzo halisi cha vidonda vilivyo. Sehemu kubwa, hufanyika kwa daktari kumuandikia dawa za kutumia na mara chache, upasuaji hufanyika.

Ni muhimu kuelewa kwamba, matibu ya vidonda vya tumbo hufanyika mara tu vinapogunduliwa na iwapo kuna vidonda vya tumbo vinavyotoka damu, mgonjwa mara nyingi analazwa, kwa ajili ya matibabu zaidi na hata kuongezewa damu inapobidi.



Pilipili, moja ya vyanzo vya vidonda vya tumbo.

Iwapo sababu ya vidonda vya tumbo itabainika kuwa ni bakteria (H. pylori) basi dawa ya kuangamiza bakteria 'antibiotic' hutumika.

Kwa vidonda vya tumbo vya kawaida, daktari hutoa dawa zinazofanya kazi ya kuzuia tumbo kuzalisha kiwango kikubwa cha tindikal.

Pia, kuna dawa nyinginezo zinazosaidia kuzuia chembehai zinazozalisha tindikali na dawa kusaidia kuweka mazingira ya tumbo vizuri kwa kupunguza ukali wake.

Dalili za vidonda zinaweza kupotea mapema, mara tu baada ya kuanza matibabu. Lakini, hata baada ya dalili kupotea mgonjwa, bado mgonjwa anapaswa kuendelea kutumia dawa alizopangiwa na daktari hadi hatua ya mwisho.

Hilo ni muhimu sana, hasa pale chanzo cha vidonda kinapokuwa ni bakteria. Inashauriwa, pia mgonjwa aliye katika matibabu asijihusishe na maumizi ya pombe, sigara, dawa na chakula kinachoamsha dalili za vidonda.

Kwa mara chache, vidonda vyenye hali ya hatari, vinachangia kufanyike tiba ya upasuaji na hiyo ni pale vidonda vinapojitokeza kila mara, havipo, vinatoa damu, vinachangia kulika kwa ukuta wa tumbo au utumbo mdogo.

Ni aina ya upasuaji unaoweza kuhusisha hatua kama: Kukiondoa kidonda chote, kuondoa nyama sehemu nyingine ya utumbo na kuziba sehemu ya kidonda na kukata mawasiliano ya fahamu ya tumbo kupunguza uzalishaji wa tindikali.

Mtu anapaswa kuelewa kwamba, kupata matibabu mapema iwezekanavyo mara tu baada ya kugundua kuwa una vidonda vya tumbo, ni jambo muhimu.

**DALILI ZAKE**

Kadri vidonda vinavyoachwa bila kutibiwa, ndivyo vinavyoleta madhara makubwa zaidi baadaye.

Mtu anapaswa kufika hospitalini haraka kumuona daktari, mara tu baada ya kupata mojawapo ya dalili zifuatazo: Kwanza, maumivu ya ghafla 'yanayokata' na hayakomi tumboni, kutoa kinyesi chenye rangi nyeusi au chenye damu au kutapika damu.

Dalili hiyo ni kiashiria kizuri kuwa kidonda kimemega sehemu ya ukuta wa tumbo au mshipa wa damu.

**KUUDHIBITI UGONJWA**

Ili kuzuia kusambaa kwa bakteria na kupunguza uwezekano wa kuwapata, watu wanapaswa kunawa mikono kwa sabuni kila mara, pia kuhakikisha chakula chao safi na kimepikwa vizuri.

Kuzuia vidonda vinavyosababishwa na matumizi ya dawa za kundi la 'Nsaid' kama aspirini. Ni busara kuepuka kwa kadri mtu anavyoweza.

Kama mtu anahitaji kutumia dawa hizo, anapaswa kuhakikisha anatumia dawa kadri ilivyopendekezwa na daktari na kuepuka matumizi ya pombe, wakati anatumia dawa za kundi hilo.

Inaelezwa, kuwapo baadhi ya tabia au mitindo ya maisha inayosaidia kuzuia watu kupatwa na vidonda vya tumbo.

Tabia hizo za kuepukwa zinajumuisha ukwepaji matumizi ya pombe, sigara, msongo wa mawazo uliopitiliza.

Hiyo yote inatajwa kusaidia kujenga ukuta wa tumbo katika hali ya uimara na wenye afya, hivyo kuondoa uwezekano wa kupata vidonda.

• ***Mawasiliano: jacpole@gmail.com***

AFYA

# Mtaalamu Mifugo anyambua viboko, mizigo, kuwafungia kunavyowatesa

## •Unajua adhabu sheria kumchapa mnyama?

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**



Punda wakibebeshwa mizigo kuliko uwezo wao. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

KATIKA jamii watu wanawafuga wanyama na inaweza kuonekana katika sura ya kufanana, lakini linapokuja swali wanawafugaje, iko wazi tofauti zinaonekana.

Pia, utamaduni wa kuishi na wanyama majumbani, una muda mrefu sana katika jamii. Hapo wanatajwa wanyama kama ng'ombe, punda, mbwa, kondoo, sungura na nguruwe.

Jambo linalojitokeza, ni kwamba kuna wanajamii wanaoishi na wanyama hao katika namna ya kuwatesa, badala ya kuishi nao kirafiki ikizingatiwa wana mchango mkubwa katika uchumi na ustawi wa maisha yao kifamilia.

**MTAALAMU MIFUGO**

Daktari Mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Godfrey Kayombo, anasema mnyama anatakiwa awepo katika makazi ya binadamu na Sheria ya Haki za Wanyama, 2007 inaeleza kuwa mnyama anatakiwa awe na mahali na alindwe dhidi ya na magonjwa.

Anataja sheria nyingine ya mwaka 2003, kwamba kuna wakati serikali ina haki ya kuua wanyama wanaozurura ovyo, wakiwamo mbwa wasio na makazi ya kulala na wanahatarisha uwezekano wa kusambaza maradhi kwa binadamu, kama kichaa cha mbwa na tatenasi.

Daktari anasema hatua huchukuliwa pale wakazi wanapoomba hatua zichukuliwe kwa mbwa wanapopunguzwa mitaani na serikali inachukua hatua stahiki, inaporidhika na hoja ya maombi.

Anafafanua kuwa, huwa anafikia hatua hiyo pale wafugaji wanaposhindwa kutimiza wajibu wao, huku akipuuza dai la kijamii kwamba anayeua mbwa anapata laana, akitumia ushuhuda binafsi wa kufanya hivyo kwa miaka 10 akibaki shwari.

**HAKI ZA WANYAMA**

Dk. Kayombo anazitaja haki za wanyama kuwa ni pamoja na nyumba, chanjo na kupewa chakula huku, akieleza kuwa asilimia 98 ya wanaofuga mbwa ni kwa ajili ya usalama.

Kumuadhibu ng'ombe au mnyama yeyote ni sahihi? Dk. Kayombo anasema ni kosa na msimamizi anatakiwa kutumia nguvu ya kawaida na anayekiuka kwa mara ya kwanza, anatozwa faini ya Sh. 50,000 na ofisa mifugo

Mtaalamu mifugo huyo, anasema wanaokiuka kwa mara ya pili na kuthibitika mahakamani wanaadhibiwa, hutozwa faini inayoanzia Sh. 300,000 hadi Sh. Sh. 500,000 au kifungo cha mwaka mmoja jela au vyote kwa pamoja kulingana na mahakama itakavyotafsiri sheria.

"Mnyama anapoadhibiwa, mishipa ya damu inapasuka na kimsingi mnyama hapaswi kupigwa sana,"anasema Dk. Kayombo, akiongeza kuwa mnyama anapopigwa, kinachovunwa mwilini ni hasara kuanzia nyama, ngozi, mbolea na maziwa.

Pia, anaeleza ubora wa nyama daima unaendana na matunzo yake, ikimchukua umri kuanzia miaka miwili hadi minne na hadi sasa, changamoto kuu inayotawala ni kuwapo uelewa mdogo wa wafugaji wanaoshindwa kuwapa haki wanyama.

**MAONI YA WAFUGAJI**

Mkazi mwingine, Riroda Martha Isaay, anasema mnyama anapochapwa hujihisi ni haki yake pale anapokosea, mfano wakati amebebeshwa mzigo na kwa maana hiyo, kuwachapa wanyama na kuwalisha chakula, liko mikononi mwa mhusika akijisikia.

Mkazi mwingine, Gallapo Bayo, anasema shida iliyopo kwa wafugaji, ni mazoea wanayoshuhudia mbwa kupatiwa chakula kichafu, pasipo kujali kwamba naye anastahili usafi, kuepushwa na maradhi. Bayo anasema, mila na desturi walizorithi ndizo zinaathiri mifugo kuendelea kuteswa kwa vipigo na kunyimwa chakula na nyumba za kuishi zilizo bora.

Mkazi wa Babati, Ernest John, anawalaumu wafugaji wanawanyima haki wanyama wanaowafuga, akiona wanadamu wanaishi maisha katika maisha duni, hivyo ni vigumu kwa kujenga tofauti hata wakawapa wanyama kilicho bora.

Mkazi wa Sinai, Neema Charles, anashauri serikali kuwa na ukaguzi kwenye makazi ya watu, kujiridhisha na hatua za usafi kwa wanyama wafugwao majumbani.

"Iwapo serikali itashindwa kudhibiti vipigo kwa wanyama wa kufugwa isitegemee mifugo inayotoka nchi yetu kuwa na thamani katika soko," anaeleza Charles

Sigino Bura, anasema upande wake hakuzijua sheria zinazowalinda wanyama kama ng'ombe, punda na mbwa na sasa ndio anasikia tetezi.

Ushauri wa Bura ni kwamba, sheria iliyopo ipo basi wataalamu wa mifugo wawasaidie kuwapa elimu ili waepuke mkono wa sheria lakini na kuwatesa wanyama na kuwafundisha njia mbadala za kuishi na wanyama hao.

Managha Buu, ana maoni dhidi ya wanaoadhibu mifugo, akiwanyooshea kidole vijana kuwa ndio wanapenda kuwaadhibu wanyama kazi.

"Unakuta ng'ombe amelima na kuchoka na analala sasa, badala ya kumuita jina lake ili kumuamsha, wanamchoma moto ili aamke," anatamka kwa kutumia mfano.

**WATETEZI WANYAMA**

Mwasisi wa Shirika la Tanzania Animal Welfare Trust Fund(PAWS), Evarest Maguo, aliyeko wilayani Arusha, anasema Sheria ya Ustawi wa Wanyama mwaka 2008, inawanyooshea kidole cha 'hapana' wafugaji kuwaadhibu wanyama.

Anazitaja haki haki tano za viumbe hao ni: Kupatiwa chakula muda wote; pili, kutosumbuliwa, akitoa mfano wa mbwa wanavyosumbuliwa kwa kupigwa mateke kila wakati.

Pia, Maguo anataja haki ya na maumivu, majeraha na magonjwa yoyote. Hapo anasema, kuna wakati ng'ombe au punda wanakuwa na maumivu na mimba, lakini bado wanafanyishwa kazi.

Anazitaja haki zingine za mifugo, kuwa inajumuisha uhuru wa mnyama kuonyesha tabia zake za asili, akitolea mfano ng'ombe anahitaji kucheza na wenzake na kuwanusa.

Maguo analaumu kwamba, wafugaji wanawachungia katika sehemu moja huku akidai wanafungwa sehemu moja mwaka mzima, akidai mnyama anapofungwa sehemu moja kwa anashindwa kujitetea, akitoa mfano inapotokea shambulio ama la nyuki au wadudu waharibifu, hawezi kujitetea.

Pia, kuna haki za uhuru wa ama akutokuwa na hofu au msongo wa aina yeyote ile.

**MENEJA PROGRAMU**

Meneja wa Programu wa Shirika la Meru Animal Welfare Organization (MAWO), Dk. Dauson Katuritsa, anasema wanaowaadhibu wanyama wana makosa, hasa katika dhana iliyozoeleka 'punda haendi bila viboko.'

Anasema, kuna alama kitaalamu ya kumwelekeza mnyama na kama vile kumpigia kipenga, ili mnyama alime au asilime.

Katika kuhakikisha jamii inabadilika, anasema sasa wanatoa elimu kwa watoto wa shule ya msingi, vyuo vya mifugo na kinamama ambao ndio watumiaji wakuu wa punda.

Uamuzi wa kuwekeza katika vyuo vya mifugo, Dk. Dauson Katuritsa, anatoa ufafanuzi kwamba unalenga kupatikana mabalozi wengi, ambao baadaye wanaajiriwa hata serikalini.

**CHAMA CHA WAFUGAJI**

Katibu wa chama cha wafugaji, wilaya ya Babati, Cassan Mallem, anapigana na wanaochaoma mifugo, kwamba wanakosea, ingawa anakiri wilaya Babati, inaongoza katika kuchapa ng'ombe, wakifuatiwa na punda.

Malle anataja kasoro nyingine ya wanyama kutumikishwa muda mrefu, akitoa mfano wa punda, kwamba zamani wazee waliwabebesha debe tano za mazao, kinyume na uwezo wao, debe tatu.

Katika kutatua kero hiyo, wameamua kutoa elimu kwa wafugaji na wanakemea adhabu kwa wanyama na kuwafanyisha kazi nyingi, kwamba ziepukwe.



Mchungaji wilayani Babati, akiwapeleka ng'ombe malishoni. **PICHA: JALIWASON JASSON**



# Watamba kumchagua JPM kwa kishindo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JUKWAA la Vijana wa Tanzania Mpya limesema vijana wana kila sababu ya kumuunga mkono Rais John Magufuli katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu kutokana na utendaji kazi wake kuwagusa wananchi, hasa wao.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Ramadhan Magambo, alisema wanaamini Rais atapitishwa na chama chake (CCM), hivyo watamuunga mkono.

"Kwa miaka mingi vijana tumekuwa tukitumika kama daraja. Zile zama za vijana kuonekana kuna umuhimu kwa kipindi fulani zimepita. Vijana tupo zaidi ya asilimia 60 nchini, hivyo tunaamini tunatosha kusema tunayemtaka," alisema.

Magambo alisema vijana bila kujali itikadi zao, kwa pamoja watamuunga mkono Rais Magufuli kama Watanzania ambao hawafungamani na chama chochote.

"Lengo sisi vijana tunataka kumpa zawadi Rais Magufuli katika uchaguzi mkuu. Hakuna Mtanzania asiyejua mema yaliyofanywa na Rais Magufuli. Tutampigia kura za kishindo na tunataka kuandika historia ya taifa letu kwamba ndiyo Rais pekee atakayekuwa amechaguliwa kwa kishindo," alisema.

Alisema watapita nchi nzima kuwafikia Watanzania ili wamchague Rais Magufuli katika uchaguzi huo.

Naye Katibu wa Jukwaa hilo, Frank Chirare, alisema Rais amepambana na vitendo vya rushwa na matokeo yake wananchi wanahudumiwa bila kutoa chochote.

Alisema amefanya mengi ikiwamo kuongeza mapato ya nchi, hivyo kuiwezesha nchi kuingia uchumi wa kati kabla ya mwaka 2025.

"Kwa hiyo hayo tuliyoyapima kwenye utendaji wake, na kiongozi tunayemtaka tumeshamwona kupitia uwajibikaji wake. Rais Magufuli amekaa ndani na kujishughulisha na mambo ya nchi yetu hakuwa mtu wa kusafiri," alisema.

Alisema wanaamini Rais anaweza kuwafikisha kule wanapotaka kutokana na utendaji kazi wake.

"Tutaenda mbele na Rais Magufuli na kuhakikisha anarudi tena Ikulu ili kuiona Tanzania bora zaidi na kufikia uchumi wa juu zaidi," alisema.



Ofisa Uchaguzi Jimbo la Dodoma Mjini, Albert Kasoga (kulia), akizungumza na washiriki kutoka vyama vya watu wenye ulemavu, viongozi wa vyama vya siasa na Jeshi la Polisi kwenye warsha kuhusu mradi wa uboreshaji wa mazingira shirikishi na wezeshi kwa watu wenye ulemavu, kwa ajili ya kujiandaa na uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka huu 2020, iliyofanyika jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Wataka kasi zaidi mapambano ukatili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuongeza mapambano ya vitendo vya ukatili kwa mwanamke hasa rushwa ya ngono mahali pa kazi ili kuwezesha mazingira ya utendaji kazi kwa ufanisi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Wanawake wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) Taifa, Beatrice Njawa, alisema hayo jana katika mkutano wao wa siku mbili.

Njawa alisema vitendo vya ukatili kwa mwanamke hasa suala la rushwa ya ngono bado lipo katika baadhi ya ofisi na imekuwa tatizo kubwa

kwao, hivyo wanaiomba serikali kuliangalia jambo hilo kwa umakini.

"Rushwa ya ngono na mfumo kandamizi bado uko kwenye ofisi zetu kupitia TALGWU tunaiomba serikali jambo hili iliangalie licha ya kwamba kwa sasa limepungua," alisema.

Alisema changamoto nyingine wanayokutana nayo ni uwakilishi mdogo katika nafasi za uwakilishi katika ngazi ya uamuzi kwa wanawake, hivyo aliiomba serikali kuweka mfumo wa pamoja kuhakikisha wanawake wanakuwa wengi katika nafasi za uongozi.

Mwenyekiti huyo alitaja tatizo lingine kuwa ni kusitishwa kwa fao la uzazi, afya na usalama mhali pa kazi.

Aidha, alisema changamoto nyingine ni mfumo wa kuchagua wategemezi katika Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) kutokuwa rafiki kwao kwa kupangiwa watu wa kupata huduma hiyo.

Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri Tanzania, Pendo Berege, alisema changamoto zote wamezipokea na watazifanyia kazi.

Alisema suala la uwakilishi mdogo kwa wanawake katika ngazi za uamuzi wamelijadili na wamekubaliana kwamba uwakilishi utaongezwa na kuonekana.

# Wasioona waomba msaada bima ya afya

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi wasioona Buigiri, Chamwino mkoani Dodoma, wamewaomba wadau mbalimbali kuwasaidia kupata bima ya afya ili kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya.

Ombi hilo lilitolewa jana na wanafunzi hao wakati wakipokea msaada wa vitu mbalimbali kutoka Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwa kushirikiana na Jumuiya ya wanafunzi wanaosomea masomo ya ualimu katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Msaada uliotolewa ni pamoja na chakula, vinywaji, sabuni na dawa mbalimbali kwa wanafunzi wa shule hiyo yenye wanafunzi wenye mahitaji maalum, inayomilikiwa na Kanisa la Anglikana Tanzania.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi hao, mmoja wa wanafunzi hao, Daniel Eliyabi, alisema pamoja na misaada wanayopatiwa wanaomba kupatiwa bima ya afya ili kuwa na uhakika wa kupata matibabu.

Mwanafunzi huyo alisema wamekuwa wakikabiliwa na uhaba wa chakula, vifaa vya kujifunzia ikiwamo mashine ya maandishi ya kawaida kwenda katika maandishi ya watu wasioona pamoja na uhaba wa walimu. "Tunaomba tuwekewe uzio kwani wakati mwingine tunajikuta tunashindwa kusoma. Tunalinda vitu vyetu kutokana na eneo hili kutokuwa na uzio, hivyo tunaiomba serikali na wadau watusaidie tupate uzio," alisema.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Samweli Jonathan, alisema wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo za ukosefu wa uzio, mazingira ya kusomea na kujifunzia kutokuwa rafiki pamoja na bajeti kutotosheleza katika chakula.

Alisema shule hiyo inaendeshwa na Kanisa la Anglikana kwa kushirikiana na serikali, hivyo aliwaomba Watanzania kuwasaidia wanafunzi hao ili watimize ndoto zao.

Naye Ofisa Elimu wa Kata ya Buigiri, Emmanuel Lotta, alisema licha ya changamoto nyingi ambazo wamekuwa wakikutana nazo shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri katika masomo yao.

"Serikali inatoa chakula tu, kuna shida ya bili za maji na umeme pamoja na kutokuwapo kwa jengo la utawala, lakini kikubwa ni mafuta kwa watu wenye ualbino," alisema.

Kadhalika, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanafunzi hao, Gerald Kwagilwa, alisema waliona ni vyema kwenda kutembelea shule hiyo pamoja na kutoa msaada wa vitu hivyo. Alisema wanafunzi hao wanakabiliwa na changamoto nyingi, hivyo wao wakiwa kama walimu watarajiwa, wameamua kwenda kuwafariji na kushirikiana nao na kuwakumbusha kuwa msingi wa kila jambo ni elimu.

Mwenyekiti huyo aliwakumbusha Watanzania na serikali kuwasaidia wanafunzi wa shule hiyo ili wapate bima ya afya kwa ajili ya matibabu itayowasaidia kupata huduma kila wanapoumwa.





## Viongozi wa mila wamchangia Tulia kugombea ubunge

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JOPO la viongozi wa mila kutoka katika Wilaya ya Rungwe, limemkabidhi Naibu Spika, Dk. Tulia Akson, fedha kwa ajili ya kuchukulia fomu za kuwania nafasi ya ubunge katika jimbo lolote analolitaka katika mkoa huo kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Viongozi hao walimkabidhi fedha hizo juzi nyumbani kwake jijini Mbeya ambapo walisema walikubaliana kumchangia fedha hizo ili zimsaidie kuchukua fomu, huku wakisisitiza kuwa hawajashawishiwa wala kulazimishwa na mtu yeyote.

Mwenyekiti wa Machifu wa Wilaya ya Rungwe, Joel Mwakatumbula, alisema waliamua kwa umoja wao kumsaidia baada ya kusikia kuwa ameshaonyesha nia ya kugombea nafasi ya ubunge katika jimbo ambalo halijawekwa wazi.

Alisema walifurahishwa na utendaji wake wa kazi katika Bunge lililopita, na ndio maana wakaamua kumsaidia fedha kwa ajili ya kuchukua fomu ili akalitumikie tena taifa.

"Huyu ni binti yetu kwa hiyo sisi kumchangia fedha kwa ajili ya fomu ni jukumu letu, tunamtakia kila la kheri kwenye kinyang'anyiro hicho, na tunaamini atafanikiwa vizuri," alisema Mwakatumbula.

Akipokea fedha hizo, Dk. Tulia aliwashukuru wazee hao kwa kujitolea kwao, na kwamba wamemsaidia kuanza safari ambayo anatarajia kuianza muda utakapotangazwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi.

Alisema uchaguzi ni mchakato ambao unahitaji kutumia fedha kwenye baadhi ya mambo, ikiwamo kuchukua fomu, hivyo fedha ambazo alipanga kuzitumia kuchukulia fomu atazitumia kwa ajili ya shughuli zingine.

"Kikanuni muda wa kuanza kuchukua fomu bado, lakini maandalizi ni muhimu, hivyo wazee wangu hawa wameona wanisaidie mapema ili pengine nisije nikakwama... nawahidi kuwa nikipata nafasi hiyo sitawaangusha," alisema Dk. Tulia.

Aliwaomba kuendelea kushirikiana naye kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo ambazo huwa anazitekeleza katika maeneo mbalimbali nchini.

# Mpango wa kuzuia malaria wazinduliwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MPANGO wa Taifa wa kutokomeza ugonjwa wa malaria kwa kuangamiza mazalia ya mbu waenezao ugonjwa huo umezinduliwa mkoani Mbeya na unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mikoa miwili ya Mbeya na Songwe kabla ya kusambaa nchi nzima.

Uzinduzi huo ulifanyika juzi jijini Mbeya na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, na unatekelezwa kwa kupuliza dawa inayotengenezwa kwenye Kiwanda cha Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC).

Mratibu wa mpango wa kutokomeza malaria nchini, Jackson Stephano, alisema mpango huo ni wa miaka mitano na unatarajiwa kufikia ukomo mwaka 2025, na kwamba wana uhakika ugonjwa huo ambao umekuwa ukigharimu maisha ya watu wengi utakuwa umetokomezwa.

Alisema kiwanda cha NDC ambacho kinazalisha dawa ya kuua mazalia ya mbu ndicho kiwanda pekee Afrika ambacho kinazalisha dawa hiyo, na kwamba baada ya kuutokomeza ugonjwa huo nchini utaratibu utaandaliwa wa kuyauzia mataifa mengine.

"Huu mpango tumeanzia katika mikoa hii miwili na uzinduzi huu utafanyika katika mikoa yote nchini, tunashukuru mikoa hii imeitikia vizuri na imekuja na azimio la kuhakikisha inatokomeza kabisa ugonjwa huu," alisema Stephano.

Alisema dawa hiyo ilishafanyiwa majaribio na ina ufanisi wa kutosha, hivyo wana uhakika kwamba ikitumika vizuri itasaidia kutokomeza ugonjwa huo kwa asilimia 100.

Meneja ubora wa Kiwanda cha NDC, Samuel Mziray, alisema dawa hiyo haina madhara yoyote kwa binadamu wala mnyama isipokuwa inaua mbu pamoja na mazalia yake, hivyo kila mdau anatakiwa kuitumia.

Alisema mapambano dhidi ya maralia kwa kutumia vyandarua na dawa zingine huwa yanalenga kukabiliana na mbu wachache na kuwaacha wengine wakiendelea kuzaliana, na kwamba wadudu hao wanazaliana kwa kasi kubwa.

"Ukitumia dawa zingine za kuua mbu ukaua mbu mmoja unakuwa umeacha watoto 1,400, ndio maana vita dhidi ya malaria nchini imedumu kwa miaka mingi bila mafanikio na inaendelea kuleta madhara, hii dawa imekuja kung'oa mzizi wa mbu hawa," alisema Mziray. Alisema vita dhidi ya malaria nchini ilianza mwaka 1890 na ilianzia katika Jiji la Dar es salaam, lakini vita hiyo haijafanikiwa, na kwamba Serikali iliamua kuanzisha kiwanda hicho ili kumaliza kabisa mbu.

Chalamila aliziagiza halmashauri zote za mkoa huo kutenga bajeti kwa ajili ya kununua dawa hiyo ili kuhakikisha mpango huo unatekelezwa kwa ufanisi.

Alisema mbu aina ya Anofelesi wanaoeneza malaria wamekuwa wakibadili tabia mara kwa mara kiasi kwamba hata njia nyingi za kukabiliana nao zikawa hazifanikiwi, na kwamba kwa kutumia dawa hiyo ya kuua viluwiluwi watatokomezwa.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Dk. Jonas Lulandala, alisema maambukizi ya malaria mkoani Mbeya ni asilimia tatu pekee, na kwamba mpango huo utasaidia wananchi na wageni wanaoingia mkoani humo kutougua ugonjwa huo.




Baadhi ya wakazi wa Mji wa Mbalizi, mkoani Mbeya, wakishuhudia ukarabati kwenye eneo la kutokea magari la stendi ya mabasi ya Tarafani juzi, ambalo lilikuwa limeharibika takribani mwezi mmoja tangu stendi hiyo ilipofunguliwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# W'biashara sokoni Kiwila walalamikia manyanyaso

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wa mazao katika Soko la Kiwira Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, wamewalalamikia baadhi ya viongozi wa Serikali kuwa wanawanyanyasa kwa kuwapiga wakilazimishwa kulipa ushuru.

Wamedai kuwa wanafanyiwa unyama huo hata pale wanapokuwa wa ma vitambulisho vya wajasiriamali vilivyotolewa na Rais John Magufuli.

Aidha, wanadai kuwa baadhi ya viongozi wanaokusanya ushuru kwenye soko hilo huwa wanawalazimisha kulipa ushuru wa mazao yao kabla hawajaingia nayo sokoni, na kwamba kwa wale ambao hawana fedha wanazuiliwa kuingia ndani ya soko hilo.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Nuru Mwaituka, ambaye ni mfanyabiashara wa mchele, alisema wanatozwa ushuru mkubwa ambao hauendani na mitaji yao, hali ambayo inasababisha wasipate faida.

Alisema wakienda kununua mchele Mbeya mjini hawatozwi ushuru, lakini wakifika Kiwira wanatakiwa kulipa ushuru hata kama mtu amebeba gunia moja, jambo ambalo anadai ni kinyume cha maelekezo ya Serikali.

"Sasa hivi mzunguko wa fedha ni mgumu, lakini tunaendelea kupambana, tatizo ni hawa maofisa wa Serikali ambao wanatunyanyasa kwa kututoza ushuru mkubwa hata kama tuna vitambulisho vya mjasiriamali," alisema Nuru.

Naye Fadhiri Sanje, mfanyabiashara wa kabichi katika soko hilo, alidai kuwa wamekuwa wakilazimishwa kulipa ushuru wa Sh. 15,000 kwa gari moja lenye uzito wa tani moja tofauti na awali ambapo walikuwa wanalipa Sh. 3,000.

Alisema kutokana na kutozwa ushuru huo mkubwa, wanalazimika kuuza mboga hizo kwa bei kubwa ili kufidia gharama za ushuru, hali ambayo inasababisha kukaa muda mrefu wakiuza mzigo ule ule.

Alimuomba Mkuu wa Wilaya hiyo, kuingilia kati tatizo hilo kwa maelezo kuwa linaathiri biashara na kudumaza uchumi wao kwa kuwa baadhi wameanza kufunga biashara sokoni hapo.

"Sisi biashara zetu tunategemeana wenyewe, soko la ndizi likiwa zuri hata sisi tunaouza kabichi tunauza na hata wauza mchele na vitu vingine wanauza vizuri... lakini kwa sasa soko la ndizi halijatengamaa kutokana na athari za ugonjwa wa corona, tunahangaika kuimarisha biashara na wengine wanatunyanyasa, tunaomba Serikali itusaidie," alisema Sanje.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara wameanza kuhama katika soko hilo na kukimbilia kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi, hali ambayo alidai inazidi kudhoofisha mzunguko wa fedha.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alipoulizwa na Nipashe, aliwataka viongozi wanaowatoza ushuru na kodi zingine wafanyabiashara wenye vitambulisho vya ujasiriamali kuacha mara moja kwa maelezo kuwa ni kinyume cha maelekezo waliyopewa.

Alisema hata wajasiriamali ambao wanastahili kuwa na vitambulisho hivyo ni wenye mitaji isiyozidi Sh. 4,000,000, na kwamba mjasiriamali anayejiona kuwa ana sifa hiyo anatakiwa akichukue kwa maofisa watendaji.

Aliwataka kuchangamkia fursa hiyo ili kuepuka kusumbuliwa na maofisa wa Serikali wanaokusanya mapato, na kwamba kwa wale ambao watatozwa ushuru wasipokuwa na vitambulisho hivyo wasimlaumu mtu.






Mwakilishi wa Viti Maalum Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kaskazini Unguja, Riziki Pembe Juma, akikabidhi printa kwa Katibu wa Umoja wa Vijana wa chama hicho (UVCCM), wilaya ya Kaskazini B Unguja, Ashura Haji, kwa ajili ya matumizi ya ofisi ya umoja huo, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ACT yaongeza muda uchukuaji fomu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KUFUATIA Tume ya Uchaguzi Zanzibar kufanya mapitio ya majimbo ya uchaguzi na hatimaye kuyaondoa majimbo manne.

Chama cha ACT-Wazalendo kimetangaza kuongeza muda wa uchukuaji fomu za kugombea ubunge, uwakilishi na udiwani hadi Julai 20 badala ya Julai 13, mwaka huu.

Hatua hiyo inatokana na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kufanya mapitio ya majimbo ya uchaguzi na hatimaye kuondoa manne.

ZEC imepunguza majimbo ya uchaguzi kutoka 54 ya awali hivyo kuyafanya kuwa 50. Majimbo yaliyoondolewa ni Chukwani, Kijitoupele, Mtopepo na Kiwengwa. Akizungumza jana wakati wa ziara yake ya kichama Mkoa wa Kaskazini Unguja, Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, alisema baadhi ya wanachama wa chama hicho walishachukua fomu lakini baada ya ZEC kukata majimbo, wamejikuta majimbo wanayotaka kugombea sasa hayatakuwapo.

Alisema kuwa hali hiyo imesababisha uchukuaji wa fomu za kugombea uongezwe ili kuwapa muda wale ambao majimbo yao yameathirika na mengine yamepunguzwa.

"Hatua hiyo ya kuongeza muda itawapa nafasi wagombea kujipanga katika safu za kugombea katika majimbo wanayoyataka," alisema.

Hata hivyo, alizitaka ZEC na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuhakikisha uchaguzi unakuwa wa huru na wa haki ili kila mmoja aridhike na uendeshwaji wa uchaguzi huo.

Maalim Seif ambaye anatarajiwa kuwa mgombea urais wa Zanzibar endapo atapata ridhaa ya chama hicho, alisema chama chake kimejizatiti na kiko tayari kwa uchaguzi.

"Hatupo tayari kuona mtu yeyote wa ACT-Wazalendo anaingia katika uongozi kwa kupitia njia ya rushwa. Hatutalifumbia macho suala hilo," alisema.

Pia aliwataka wanawake kugombea katika majimbo ili kuongeza uwakilishi wa wanawake katika vyombo vya uamuzi.

katika hatua nyingine, Maalim Seif akiwa katika ziara yake, alisema anaamini Rais John Magufuli atahakikisha uchaguzi unakuwa wa huru na haki.

# Raza atoa neno uteuzi wagombea CCM

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Jimbo la Uzini, Mohamed Raza, ameuomba uongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) chini ya Mwenyekiti wake, Rais John Magufuli, kuwatathmini kwa makini wanachama ambao wataomba ridhaa ya kugombea nafasi za uongozi kuelekea uchaguzi mkuu. Raza aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kutangazia umma kuwa atagombea tena Jimbo la Uzini kupitia CCM ili kuwaongoza tena wananchi wa jimbo hilo. Alisema wako baadhi ya wanachama wameyakimbia majimbo yao na kushindwa kuwatumikia wananchi, hivyo ni vyema chama kuwatathmini kwa kina ili wananchi waendelee kuwa na imani ya chama hicho.

Kwa mujibu wa Raza, kuwapitisha wagombea ambao hawakuleta maandeleo katika majimbo kutasababisha kukikandamiza chama kuelekea uchaguzi mkuu.

Raza alisema licha ya kwamba atagombea tena, aliwataka wana CCM wenzake ambao wana nia ya kuomba nafasi hiyo, kujitokeza katika kuchukua fomu. Pia alitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutekeleza ahadi yake ya ujenzi wa barabara za ndani ambazo tayari ameshachangia Sh. milioni 20 ikiwa ni hatua ya kusaidia ujenzi huo uliothaminiwa kugharimu Sh. milioni 80.

"Bado zipo barabara za ndani hasa katika Jimbo la Uzini ambazo hazijakarabatiwa na serikali hii iliyopo madarakani iliahidi kuzikarabati ili kuwaondoshea usumbufu wananchi," alisema Raza.

# SMZ yataka kazi ujenzi wa uwanja

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeiagiza kampuni ya BCEG inayojenga jengo la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Karume kuhakikisha inakabidhi mradi huo ndani ya kipindi hiki cha serikali ya awamu ya saba kabla haijaondoka madarakani.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mohammed Ahmada Salum, alisema hayo jana alipofanya ziara katika uwanja huo kuangalia maendeleo na hatua iliyofikiwa.

Alisema ni vyema kampuni hiyo ikahakikisha kipindi hiki kifupi kilichobaki inafanya kazi usiku na mchana ili kumpa heshima Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, kufungua jengo hilo.

"Nataka kuona mnafanya kazi usiku na mchana na inapofika Septemba mkabidhi serikalini na kufunguliwa na Rais wetu kwa ajili ya kuanza kazi," alisema.

Alisema kukamilika kwa ujenzi huo utaweza kuleta manufaa makubwa kwa wananchi wa Zanzibar ikiwamo kuongeza idadi ya watalii wanaoingia nchini na fursa za ajira kwa vijana.

Naibu Waziri huyo alisema zaidi ya Sh. bilioni 60 zimetumika kwa ajili ya mradi huo, hivyo ni vyema kampuni hiyo ikahakikisha inakamilisha ujenzi huo kwa wakati.

Naye Meneja wa Mradi huo, Yaser de Costa, alitaka kupatiwa wafanyakazi wazalendo katika baadhi ya sehemu ya ujenzi huo ili kutimiza lengo la serikali ifikapo Septemba wawe washakamilisha.

Alisema hivi sasa uwanja huo umefikia hatua nzuri, hivyo kupatikana kwa wafanyakazi ni chachu ya kukamilisha ujenzi huo kwa muda uliopangwa.

Mhandisi kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ya Serikali ya Tanzania, Rehema Miyeya, alisema ujenzi huo umefikia asilimia 55 na wanatarajia mwisho wa mwezi huu utakamilika.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba inauzwa ina ghorofa moja, ina godown ina fremu 10 na ina eneo kubwa wazi, ipo Dar es Salaam. Mawasiliano 0757 079057


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA VYETI



**DEOGRATIUS JUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1310-0082** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia TABATA SEKONDARI mwaka 2006. Cheti cha marudio ya kidato cha nne chenye index namba **P0337-0038** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia NAVY J.W.T.Z CENTRE mwaka 2007.

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**Taarifa ya polisi: OB/RB/209/2016.**

158027

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Rehema Hard Ngwale** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Toyota Hiace yenye namba za usajili T 990 DDK chasis namba RZH 1830003169 injini namba 2RZ 3042564.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Taarifa ya polisi RB. Namba IR/IR/RB/1158/2020.**

158026

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Nancy Emilly Kisamo** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Toyota IST yenye namba za usajili **T212 DDW,** chasis namba NCO600138741, injini namba **2NZ3007624.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Taarifa ya Polisi RB: DAR/SEL/RB/513118/2020**

158014

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO
TANGAZO LA KUITWA SHAURINI

SHAURI LA TARAKA NAMBA:58..2020

| | |
|---|---|
| Mdai: | ASHA MOHAMED |
| | DHIDI YA |
| Mdaiwa: | KILIA MOHAMED |
| Kwa: | KILIA MOHAMED |
| Ombi la Mdai: | ASHA MOHAMED |
| Madai ya: | TARAKA MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA MTOTO TSH.50,000/= |

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe **09 mwezi 07 mwaka 2020 saa 02:30 Asubuhi.**

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 06 mwezi 07 mwaka 2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

158031

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo:
MJINI-MOROGORO
**Usimamizi wa mirathi No;164/2020**

Ombi la HUSNA HARUNI MCHUMA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAROUN ALLY MCHUMA Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 09/07/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 30/06/2

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

158030

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOSEPH JACKSON SHONGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T.212 ANH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.Taarifa ya polisi **MBE/MBE/514983/2020.**

115804002

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

GODLIVER GEROLD NGATUNGAanatangaza kupotelewa na kadi ya PIKIPIKI aina ya BAJAJ BOXER yenye namba za usajili MC 371 BUP, Chassis namba MD2A21B9HWF94410, Engine no PFZWHF46820.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/504258/2020.

158037

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)
Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI

**Usimamizi wa Mirathi Na. 67/2020**

Ombi la **ALI MAHSEIN HAIDARI** kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **MAHSEIN HAIDARI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 20/7/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 03/07/2020.

158036

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)
Katika Mahakama ya Mwanzo ya MBAGALA

Usimamizi wa Mirathi Na. 190/2020
Ombi la MOHAMED MBARAKA NGAMBA kuteuliwa

Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu
MBARAKA ALLY NGAMBA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 14/07/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 29/06/2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MBAGALA

158034


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mkurugenzi FBI: China ni tishio kubwa kwa Marekani

**WASHINGTON, Marekani**

MKURUGENZI wa Shirika la FBI nchini Marekani, Christopher Wray, amesema kwamba vitendo vya upelelezi na wizi unaotekelezwa na Serikali ya China ni tishio la muda mrefu kwa Marekani.

Akizungumza katika Taasisi ya Hudson mjini Washington, Wray alielezea kampeni ya usumbufu iliyokithiri.

Alisema kwamba China imeanza kuwalenga raia wake wanaoishi ughaibuni, ikiwashurutisha kurudi nyumbani na kwamba ilikuwa inajaribu kuingilia utafiti wa corona wa Marekani.

"China imeanza juhudi za kuhakikisha kuwa ndio taifa la pekee litakalokuwa na uwezo mkubwa zaidi duniani kwa hali na mali," alisema Wray.

Katika hotuba iliyodumu kwa muda wa saa moja, Wray alieleza namna China inavyoingilia masuala ya Marekani kupitia kampeni kubwa ya upelelezi wa uchumi wa Marekani, wizi wa data na fedha kwa lengo la kushawishi sera za Marekani.

"Tumefikia wakati ambapo FBI sasa imeanza kufungua kitengo cha kukabiliana na visa vya ujasusi wa China kila baada ya saa 10," alisema Wray na kuongeza:

"Kati ya visa 5,000 vya kukabiliana na ujasusi vinavyoendelea kote nchini, karibia nusu yake vinahusishwa na China," alisema Wray.

Mkurugenzi huyo aliongeza kuwa Rais wa China, Xi Jinping alianzisha mpango kwa jina 'Fox Hunt', unaowalenga raia wa China walioko ughaibuni wanaoonekana kuwa tishio kwa serikali ya nchi hiyo.

"Tunazungumzia kuhusu wapinzani wa kisiasa, watoro na wakosoaji walio na lengo la kufichua ukiukaji wa haki za kibinadamu unaotekelezwa na China. Serikali ya China inataka kuwalazimisha kurudi nyumbani na mbinu zinazotumiwa na China kufanikisha mpango huo inashtua," alisema Wray.

Aliendelea: Inaposhindwa kumpata mtu inayemtafuta, serikali ya China hutuma mjumbe kutembelea familia ya mtu huyo nchini Marekani. Ujumbe unaotolewa ni: Rudi China haraka ama ujiue.

***BBC***




Baadhi ya wanaharakati nchini Kenya wakiwa wamepiga magoti huku wakishika mabango wakati wa maandamano, wakilalamikia ukosefu wa haki nchini humo. **PICHA: REUTERS**

# Kenya yatangaza kufungua shule mwakani

**NAIROBI, Kenya**

WIZARA ya Elimu nchini Kenya imetangaza kuwa shule za msingi na sekondari zitafunguliwa mwaka 2021.

Waziri wa Elimu Profesa George Magoha, alisema mitihani ya kitaifa sasa haitafanyika mwaka huu kutokana na athari iliyosababishwa na ugonjwa wa virusi vya corona.

"Tulikuwa tumepanga wanafunzi wa darasa la nane na kidato cha pili warudi shuleni, lakini tumebadili wazo hilo," alisema Magoha.

Waziri Magoha alisema uamuzi huo ulifikiwa kufuatia majadiliano ya kina yaliojumuisha wadau wote katika sekta ya elimu.

Alisema: "Shule zitafunguliwa endapo idadi ya maambukizi kwa siku itapungua kwa siku 14 mfululizo".

Alisema vyuo vikuu navyo vitafunguliwa kwa awamu, lakini wasimamizi wametakiwa kuzingatia mwongozo wa kinga uliotolewa na Wizara ya Afya.

Magoha alisema vyuo ambavyo vitakiuka mwongozo huo vitafungwa.

Juzi, Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta aliondoa masharti ya usafiri wa kuingia na kutoka katika miji ya Nairobi, Mombasa na Mandera Kaskazini mwa nchi.

Rais Kenya aliwatahadharisha kutolegeza juhudi za kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa wa corona akisema kuwa ni juhudi ya mtu binafsi.

Licha ya kuondolewa kwa marufuku ya usafiri, Wakenya bado wametakiwa kuzingatia kauli ya kitaifa ya kutotoka nje nyakati za usiku. Juzi Rais Kenyatta pia alitangaza kuwa safari za ndege ndani ya Kenya zitaanza tena Julai 15, mwaka huu kwa kuzingatia miongozo na kanuni kutoka kwa wataalamu wa afya kutoka Wizara ya Afya na mamlaka ya usafi wa anga nchini humo.

Safari za kimataifa za kuingia na kutoka nchini zitaanza Agosti mosi, mwaka huu.

Wanasayansi nchini Kenya wanakadiria kwamba huenda Wakenya milioni 2.6 tayari wana virusi vya corona, hayo yamejitokeza baada ya wanasayansi kupima damu iliyotolewa kwa ajili ya protini inayotumika kwenye mfumo wa kinga.

Kwa mujibu wa data ya utafiti wa Taasisi ya Matibabu Kenya pamoja na Taasisi ya Afya ya Welcome Trust, takribani watu 550,000 sawa na asilimia 12. 4 ya wakazi wa Nairobi tayari walikuwa wamejenga kinga ya mwili kabla ya kutangazwa kwa mgonjwa wa kwanza wa corona nchini humo.

Katibu Mkuu wa chama cha madaktari nchini Kenya (KMPDU), Dk. Chibanzi Mwachonda, anaonya kuwa hali ya huduma hospitalini ni tete.

"Kumekuwa na ongezeko la maambukizi katika mwezi wa Juni na Julai, lakini kumekuwa na shinikizo kutoka wa wananchi la kufunguliwa tena kwa shughuli za kiuchumi," alisema Dk. Mwachonda. ***BBC***

## Marekani yaanza mchakato kujitoa WHO

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameanza mchakato wa kuiondoa rasmi nchi yake kwenye uanachama wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Rais Trump, Mei, mwaka huu aliweka bayana nia hiyo akiishtumu WHO kwa kutumika na China katika mapambano ya ugonjwa wa corona, na sasa ameandikia Umoja wa Mataifa (UN) na Bunge la Congress kuhusu mchakato huo.

Kujiondoa huko kwa Marekani kumepangwa kufanyika Julai 6 mwakani, kwa mujibu wa vyanzo kadhaa.

Rais Trump alilishutumu WHO kwa kuruhusu ugonjwa wa corona kushindwa kudhibitika na kupuuzia hatari ya ugonjwa huo, ambao umesababisha vifo vya maelfu ya watu duniani.

Rais Trump aliilaumu China kwa kujaribu kuziba mlipuko huo na kuishtumu WHO kwa kushindwa kuiwajibisha China.

Pia alilishutumu shirika hilo kwa "kuipendelea China", sehemu ya shutuma hizo zikiwa ni kutokana na upingaji wake mkali wa hatua ya Marekani kuwazuia wasafiri kutoka China kuingia nchini humo.

Mei, mwaka huu Rais Trump alitangaza kwamba Marekani itasitisha kulichangia shirika hilo na kutumia fedha hizo kwa ajili ya shughuli zingine.

Marekani ni mchangiaji mkubwa wa WHO. Taarifa rasmi ya kujiondoa huenda ikaathiri juhudi za dunia za kupambana na maambukizi ya virusi hivyo.

**RFI**

## Rais wa Brazil akutwa na corona

**BRASILIA, Brazil**

RAIS wa Brazil, Jair Bolsonaro, ambaye kwa muda mrefu amekuwa akiipuuza miongozo ya kujikinga na virusi vya corona amepimwa virusi hivyo na kukutwa na maambukizi.

Hatua ya kumpima Rais Bolsonaro imekuja bada ya kuonyesha dalili ikiwamo kupata homa.

Rais Bolsonaro ambaye mara kwa mara alikuwa akikataa kuvaa barakoa, alisema pia amechunguzwa mapafu kwa kutumia kipimo cha picha cha X-ray katika hospitali ya kijeshi kama tahadhari.

"Ninaepuka kuwakaribia watu, kwa sababu nimetoka hospitali kupima corona na nimegundulika nimeathirika, lakini najisikia vizuri. Asilimia 90 ya watu watakaoambukizwa hawatokuwa na dalili. Tunachopaswa kufanya ni kutovieneza virusi kwa wengine. Iwapo nitaathirika virusi vya corona, sitokuwa na wasiwasi," alifafanua Bolsonaro.

Rais huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 65, alisema amekuwa akitumia dawa ya hydroxychloroquine, kama hatua za kujikinga.

**DW**



## SARRI AGEUKA MBOGO JUVE IKIZAMISHWA NA MILAN

**TURIN, Italia**

KOCHA wa Juventus, Maurizio Sarri, ameilaumu timu yake kwa "kuangukia pua" baada ya vinara hao wa Serie A, kukumbana na kipigo cha kushitua cha mabao 4-2 kutoka kwa wapinzani wao wa Ligi Kuu ya Italia, AC Milan.

Juve walionekana wapo kwenye nafasi ya kushinda kwenye mchezo huo uliopigwa dimba la San Siro, wakati walipopata mabao mawili ndani ya dakika sita kutoka kwa Adrien Rabiot na Cristiano Ronaldo na kuwapa uongozi wa 2-0 kwa kipindi cha dakika 53.

Hata hivyo, Milan walipindua meza kwenye mchezo huo wa Jumanne, wakifunga mabao matatu ndani ya dakika tano na kuchukua uongozi wa 3-2 kabla ya Ante Rebic kuongeza bao la nne zikiwa zimesalia dakika 10 mchezo kumalizika.

"Nafikiri dakika zetu 60 za kwanza tulikuwa kwenye kiwango bora cha dunia. Tulikuwa kwenye utawala na tukakutana na anguko hili," amesema Sarri akiiambia DAZN.

"Huwezi kufikiri sana, kwa sababu tuna mchezo mwingine ndani ya siku tatu zijazo.

"Tulipata anguko ndani ya dakika 15. Inatokea kwa timu nyingine kwa kipindi kama hicho. Tunatakiwa kuchukua kwa mtazamo chanya mchezo huu, kwamba tunatawala karibia saa moja, halafu tunaanguka.

"Mara zote haiwezekani kutafuta sababu ya kipigo kama hiki, kwa hakika ni jambo linaloshangaza wakati mwingine."

## ARTETA: WACHEZAJI ARSENAL HAWAJIFUNZI

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amesema kwamba, Arsenal lazima ijifunze kumaliza mchezo kwa ufanisi wakati wanapokuwa kwenye nafasi ya kuzifunga timu za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya England.

Bao la Jamie Vardy la dakika ya 84 lilizima ndoto za Arsenal kuibuka na ushindi dhidi ya Leicester City kwenye mchezo uliopigwa katika dimba la Emirates, Juni Jumanne.

Walionekana kuwa kwenye nafasi ya kuibuka na ushindi baada ya kupata bao la kuongoza la Pierre-Emerick Aubameyang katika kipindi cha kwanza, lakini walikatishwa na kushindwa kupanda nafasi ya sita.

Hata hivyo, kadi nyekundu ya Eddie Nketiah iliwafanya Arsenal kubakiwa na wachezaji 10 uwanjani zikiwa zimesalia dakika 15 mchezo kumalizika, na kocha Arteta aliachwa akiwa na hasira.

"Tunatakiwa kujifunza. Unapocheza na timu ambyo tayari umeshaitawala unatakiwa kumaliza mchezo haraka," alisema Arteta akiwambia waandishi wa habari.

"Hii ni mara ya nne tunajikuta tukitakiwa kucheza na wachezaji 10 uwanjani. Haiwezekani kuendelea kucheza kwa staili hii. Na sikupenda namna tulivyoruhusu bao.

"Ni vigumu kufanya hivyo. Kitu kigumu ni kufunga mabao. Tulitengeneza nafasi na tulikuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kushinda. Lakini tulishindwa kumaliza mchezo kwa haraka."

Arsenal sasa italazimika kuhakikisha inashinda mchezo wake wa Jumapili dhidi ya Tottenham ili kuweka hai matumaini ya kufuzu kucheza michuano ya Ligi ya Europa msimu ujao.

# PULISIC AZIDI KUNONA CHELSEA

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amemsifia Christian Pulisic baada ya nyota huyo aliyepo kwenye kiwango bora kufunga tena Jumanne, wakati wakiibuka na ushindi dhidi ya Crystal Palace kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Pulisic alifunga bao lake la nane msimu huu katika mechi 16 alizoanza na la tatu tangu kurudi tena kwa msimu baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, wakati Chelsea ikiibuka na ushindi wa 3-2 pale kwenye dimba la Selhurst Park.

Baada ya Olivier Giroud kufunga bao la ufunguzi dakika ya sita, Pulisic alifunga la pili dakika ya 27, kabla ya Wilfried Zaha kuwafungia nyota wa Palace.

Lakini Tammy Abraham alifunga bao la pili dakika ya 71 kuwahakikishia Chelsea kupanda juu ya Leicester City katika nafasi ya tatu kwenye msimamo, licha ya Christian Benteke kufunga la pili.

Lampard alimsifia nyota huyo wa kimataifa wa Marekani, Pulisic - ambaye aliwasili hapo akitokea kwa miamba wa Bundesliga, Borussia Dortmund, mwanzoni mwa msimu huu akimfananisha na nyota wa zamani wa Blues hao, Eden Hazard.

"Sikuweza kuachana kumtumia (Christian Pulisic). Nilijua kipaji alichonacho na nilitaka kumsaidia yeye wakati alipotua hapa kwa mara ya kwanza, kwa sababu hii ni ligi ya kutumia nguvu, na nafikiri ni ligi bora kwa sababu ya nguvu ya asili," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari.

"Anaweza kuingia akitokea benchi na kufanya vizuri, mwanzo niliweza kumfanya asiwe anaanza, lakini sasa anaonekana yuko fiti na naweza kutusaidia."

# DILI LA NEYMAR BADO GUMU

**BARCELONA, Hispania**

UWEZEKANO wa Neymar kurudi Barcelona kutoka Paris Saint-Germain "ni mdogo", kwa mujibu wa Rais wa Klabu hiyo la LaLiga, Josep Maria Bartomeu.

Fowadi huyo wa kimataifa wa Brazil aliondoka pale Camp Nou kwenda kwa miamba hao wa Mji Mkuu wa Ufaransa kwa ada iliyoweka rekodi ya euro milioni 222 mwaka 2017, lakini kurudi Barcelona - ambako alishinda mataji nane kwa misimu minne aliyokaa- inaonekana ni ngumu.

Bartomeu anafikiri kwamba kutakuwa na ugumu kwa klabu yake kumsajili mchezaji huyo, hasa kutoka na klabu nyingi Ulaya kuathirika kifedha na mlipuko wa virusi vya corona.

"Mpango huu ni mdogo kwa sababu ya hali ya klabu zilivyongumu barani Ulaya," alisema Bartomeu akiiambia RAC 1.

Bado hakukanusha wakati Bartomeu alipoulizwa kuhusu usajili wa fowadi mwingine, Lautaro Martinez.

Mchezaji huyo mwenzake na Messi kwenye timu ya taifa ya Argentina, anatajwa kuwa ada yake ni euro milioni 111 ili kumng'oa pale Inter Milan.





## GUARDIOLA ATAKA MESSI ABAKI BARCELONA

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amerudia kusema anataka kuona Lionel Messi anabaki kwa miamba wa Katalunya, Barcelona.

Nyota huyo wa Barca, Messi mkataba wake unamalizika mwaka 2021 na kuna uvumi kwamba mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or anaweza kuamua kuondoka kwenye klabu hiyo ambayo haijashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu mwaka 2015.

Fowadi huyo mara kwa mara amekuwa akihusishwa na kuhamia Manchester City kucheza chini ya kocha wake wa zamani pale Camp Nou, Guardiola.

Lakini bosi huyo wa City hakuwa tayari kuzungumzia kuhusu uhamisho huo kuelekea mchezo wake wa jana Jumatano wa Ligi Kuu England dhidi ya Newcastle United.

Na pia alibainisha mtazamo wake kwa Messi haujabadilika, akiwa awali alisema matumaini yake ni kuona nyota huyo wa kimataifa wa Argentina anabakia pale Barca wakati alipoulizwa kuhusu swali hilo.

"Sitazungumza kuhusu uhamisho hadi mwishoni mwa msimu," alisema.

"Matarajio yangu ni kwamba Messi atabakia Barcelona."

## ATLETICO YAMKUNA MORATA

**MADRID, Hispania**

ALVARO Morata amesema Atletico Madrid wanakaribia kufikia malengo yao kwenye LaLiga wakati wakiwa kwenye nafasi nzuri ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Atletico ipo kwenye nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, baada ya Jumanne kutoka sare ya kufungana 1-1 na Celta Vigo.

Morata alifunga bao la haraka zaidi kwenye LaLiga msimu huu katika sekunde ya 51, kwenye mchezo huo uliopigwa kwenye dimba la de Balaidos, ambapo Fran Beltran alisawazisha mapema kipindi cha pili.


Atletico hawajafungwa katika mechi 15 na wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo, tatu zaidi ya Sevilla na tisa zaidi ya Villarreal - ambapo wote wamebakiwa na mechi nne.

Morata ndio mchezaji anayeongoza kwa kufunga mabao kwa Atletico kwenye LaLiga msimu huu akiwa na 11, lakini fowadi huyo amejiwekeza zaidi kwenye malengo ya timu, huku wakiwa wameshatinga robo fainali ya ligi ya mabingwa Ulaya kabla ya mlipuko wa virusi vya corona.

"Haijalishi (kuhusu kuwa mfungaji bora wa timu), hii ni timu, unatakiwa kuendana na malengo ya timu," alisema Morata akiiambia Movistar.

"Na halafu unaweka kichwa chako kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# DE GEA ANAWEZA KUCHEZA MIAKA 10 ZAIDI – SCHMEICHEL

●●●Asema ni mtu aliyeisaidia Man United, anapitia wakati mgumu lakini...

**MANCHESTER, England**

PETER Schmeichel amesisitiza David de Gea ni golikipa sahihi kwa Manchester United na anaweza kucheza kwa muongo mwingine.

Kiwango cha De Gea kimekuwa kizungumzwa zaidi siku za hivi karibuni, huku golikipa huyo wa Hispania akisuasua kufikia kiwango ambacho kulimfanya kuwa mmoja wa makipa bora duniani.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 29 alifanya makosa mengi kwa United, likiwamo kosa dhidi ya Tottenham na mchezo kumalizika kwa sare ya 1-1 ambapo mchezaji mwenzake wa zamani na Schmeichel, Roy Keane akaibuka na kumbwatukia.

Hata hivyo, gwiji wa United, Schmeichel, amempa sapoti yote kipa huyo wa zamani wa Atletico Madrid.

"Ni mtu wa aina yake kwa upande wetu, hakuna shaka kuhusu hilo," alisema Schmeichel akiiambia MUTV.

> **"Amepitia kwenye wakati mgumu katika soka la kisasa kwenye histori ya Manchester United. Amekuwa akipanda na kushuka, hilo ni jambo la kawaida, yeye ndio mchezaji wetu bora.**

"Hakuna shaka kuhusu hilo. Kwa miaka mitano amekuwa mchezaji wetu bora wa mwaka. Suala la kiwango chake ni la kawaida na amekuwa akifanya vizuri kwa klabu.

"David ni kipa wetu namba moja - bado ni kijana, ana wakati mzuri unaokuja.

"Anaweza kucheza kwa miaka mingine 10. Tumuunge mkono. Tunatakiwa kumpa sapoti kwa kile tulichonacho kwa sababu tunajua tulichonacho ni kizuri sana."

"Ni rahisi kumlaumu golikipa, lakini mimi siwezi kufanya hivyo," aliongeza kusema Schmeichel.

"Najaribu kusema kwamba, kila golikipa anahitaji kulindwa na hakuna shaka kwa namna anavyocheza na timu ilivyo, anatakiwa kuwa kwenye kiwango cha kumpa sapoti zaidi.

"Hatari nyingi ambazo amekuwa akiokoa zimekuwa zikifanywa na safu yote ya ulinzi, hivyo haipaswi kulaumiwa yeye peke yake.

## KWA UFUPI

**MAN CITY, JUVE ZAMWANIA TRAORE**

MANCHESTER City na Juventus wamekwenda mbele ya Barcelona katika kumshawishi winga wa Wolves na Hispania, Adama Traore mwenye umri wa miaka 24. ***(ESPN)***

**CHELSEA YAJIWEKA KWA HAVERTZ**

CHELSEA ipo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili fowadi wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 21, huku klabu nyingi zimekatishwa tamaa na bei iliyotajwa na klabu hiyo ya Ujerumani ya pauni milioni 90. ***(Goal)***

**JORGINHO KUTIMKA CHELSEA**

KIUNGO aliyekosa namba pale Chelsea, Jorginho mwenye umri wa miaka 28, anaondoka kipindi cha majira ya joto ili kurahisisha usajili wa Kai Havertz. ***(Mirror)***

**BARCA YAJITOSA KWA NDOMBELE**

BARCELONA imeonyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa Tottenham na Ufaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 23, na mlinzi wa Uingereza, Ryan Sessegnon mwenye umri wa miaka 21 atakuwa sehemu ya dili hilo. ***(Evening Standard)***

**MAN YAPEWA MUDA KWA SANCHO**

KLABU ya Borussia Dortmund imeitaarifu Manchester United kuwa Agosti 10 kuwa ni siku ya mwisho ya kukamilisha usajili wa winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20. ***(Mirror)***

**ABRAHAM ATAKA MSHAHARA MPYA**

FOWADI wa England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 22, ameiambia Chelsea anataka mkataba mpya ambao utamfanya alipwe pauni 130,000 kwa wiki. ***(Times)***

**MOYES AWAWINDA JONES, LINGARD**

KOCHA wa West Ham, David Moyes anafikiria kuwasajili nyota wawili wa England wanaocheza pale Manchester United, Phil Jones mwenye umri wa miaka 28, na Jesse Lingard mwenye miaka 27. ***(Independent)***

**UNAI AGOMBEWA EPL**

ARSENAL, West Ham na Everton zote zimeonyesha nia ya kumtaka mlinzi wa Athletic Bilbao na Hispania, Unai Nunez mwenye umri wa miaka 23. ***(AS, via Sport Witness)***

**STURRIDGE NI UFARANSA AU MAREKANI**

STRAIKA wa zamani wa England, Daniel Sturridge angependa kwenda kucheza kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1 au Ligi Kuu ya Marekani, ~~MLS. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30~~ kwa sasa ni mchezaji huru. ***(L'Equipe)***

**ETIENNE KUMBAKIZA SALIBA**

KLABU ya Saint-Etienne ina matumaini ya kumbakiza mlinzi wa Arsenal, William Saliba mwenye umri wa miaka 19 anayecheza hapo kwa mkopo, kwa ajili ya fainali ya kombe la Ufaransa, licha ya kutofikiwa makubaliano ya kuongeza mkataba huo wa mkopo kwa pauni milioni 2.3. ***(Mirror)***

**CHONG KUONDOKA MAN UNITED**

WINGA wa Uholanzi, Tahith Chong mwenye umri wa miaka 20, anaweza kuondoka Manchester United kwa mkopo msimu ujao, kwa mujibu wa wakala wake. ***(Stretty News)***

**GRIEZMANN KUBAKIA BARCELONA**

BARCELONA imemhakikishia straika wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 29, yupo kwenye mipango yao msimu ujao. ***(L'Equipe)***



HABARI MICHEZO

# TAIFA STARS WAKUNWA UDHAMINI WA SERENGETI

Na Mwandishi Wetu

WACHEZAJI wa Timu ya Taifa, Taifa Stars, wameelezea kufurahishwa na udhamini wa bia ya Serengeti Premium Lager na kusema umekuwa chachu kubwa kwa mafanikio ya timu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wachezaji hao wamesema udhamini huo umewafanya wachezaji kucheza kwa kujituma na bidii katika kuhakikisha Stars inafanya vizuri.

Mshambuliaji, John Bocco alisema, udhamini wa Bia ya Serengeti umeiwezesha timu kupiga hatua kubwa ikiwa ni pamoja na kufuzu kucheza Mashindano ya Mataifa ya Afrika (AFCON) mwaka jana, baada ya miaka 39 tangu ifuzu mara ya mwisho.

"Mpira unahitaji uwekezaji ili kupata mafanikio. Kampuni ya bia ya SBL kupitia bia yake ya Serengeti imeweza kutoa udhamini ambao umekuwa chachu kubwa katika kuimarisha timu yetu ya taifa. Pengine kama siyo udhamini huu tusingeweza kufika hapa tulipofika leo," alisema Bocco.

Kwa upande wake, Frank Domayo alisema udhamini huo umefanikiwa kujenga umoja na uzalendo kwa mashabiki, jambo ambalo limekuwa likiwapa hamasa kubwa wachezaji.

"Mdhamini amefanya kazi kubwa kuwaleta Watanzania pamoja na kuhamasisha uzalendo kwa timu yao ya taifa kupitia vyombo vya habari na kampeni zinazowahusisha wachwzaji moja kwa moja," alisema kiungo huyo.

Domayo aliongeza kuwa mdhamini amekuwa akifanikisha maandalizi mazuri kwa kuhakikisha kuwa mahitaji ya wachezaji na timu kwa ujumla yanapatikana kwa uhakika na kwa wakati pia.

"Tumeona tofauti kubwa wakati bia ya Serengeti ikiwa mdhamini wa timu yetu ya taifa. Tumekuwa tukikaa kwenye hoteli nzuri tunaposafiri na tunapokuwa kambini na hata maslahi yetu sisi wachezaji yameboreshwa kwa kiasi kikubwa jambo ambalo limetufanya tujitume zaidi," alisema.

Beki wa kulia wa timu hiyo, Erasto Nyoni alisema mdhamini huyo kwa kiasi kikubwa amekuwa karibu na wachezaji jambo ambalo limekuwa likiwatia moyo.

"Mdhamini amekuwa na timu siyo tu ndani ya uwanja bali hata nje ya uwanja kwa kutupa hamasa na hili limekuwa likiwajenga vyema wachezaji kisaikolojia," alisema Nyoni.

Naye mlinda mlango wa timu hiyo, Mechata Mnata alisema mdhamini amekuwa akijitahidi kuipa timu kila aina ya ushirikiano na hivyo kufanya maandalizi yawe mazuri na kuweza kufanya vizuri katika mechi zake

Kampuni ya SBL kupitia Bia ya Serengeti ilikuwa mdhamini mkuu wa timu ya taifa kuanzia mwaka 2017 baada ya kusaini mkataba wa miaka 3 na Shirikisho la Mpira wa Miguu hapa nchini (TFF).




Watoto wanaookota mpira wakinawa kabla ya kuanza kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Simba na Namungo kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani Lindi jana. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Namungo yaleta mapinduzi Bara

Na Somoe Ng'itu, RUANGWA

IKISHIRIKI Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Thierry Hitimana, amesema timu yake imefanikiwa kuleta mapinduzi kwenye ligi hiyo ambayo hutoa mwakilishi wa nchi katika mashindano ya kimataifa.

Akizungumza na Nipashe mjini hapa, Hitimana alisema kikosi chake kimeleta mabadiliko na kuongeza ushindani katika Ligi Kuu Tanzania Bara katika msimu wake wa kwanza.

Hitimana alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kupambana katika kila mechi waliyocheza na kufanikiwa kutimiza malengo yao wa asilimia zaidi ya 80.

Kocha huyo alisema haukuwa msimu rahisi, lakini juhudi za pamoja za viongozi, wachezaji na wadau wa timu hiyo zimesaidia kufanya vema na ikiwa ni moja ya timu zinazoogopewa.

"Tumefanikiwa kufanya vizuri na kuamsha wengine, tumeleta mapinduzi katika Ligi Kuu, naamini tumekosa ubingwa, lakini tuna nafasi ya kupata tiketi ya kwenda kushiriki mashindano ya kimataifa ya CAF (Shirikisho la Soka Afrika)," Hitimana alisema.

Kutokana na kuipa mafanikio Namungo FC, kocha huyo anatajwa kuwindwa na Yanga, ili kuungana na Mbelgiji Luc Eymael kwa mara nyingine.

Namungo iko katika hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la FA, itavaana na Sahare All Stars Jumapili mchana wakati jioni Simba itapambana na Yanga.

## Eymael: Hatuna hofu na Simba

Na Faustine Feliciane

KOCHA wa Yanga, Luc Eymael, amesema kuwa licha ya mchezo wao wa Jumapili wa nusu fainali ya kombe la FA kuwa muhimu sana kwao hawana presha na hofu na Simba.

Yanga itavaana na Simba kwenye Uwanja wa Taifa kuanzia saa 11:00 jioni kwenye mchezo huo wa nusu fainali ya kombe la FA.

Eymael alisema kuwa amewataka wachezaji wake hao kutokuwa na presha na mchezo huo kwa kuwa ni mchezo kama michezo mingine.

Amesema kuwa anaendelea kuweka mipango yake sawa kuelekea kwenye mchezo huo, lakini hawana presha na Simba.

"Mchezo utakuwa mzuri kwa sababu ya ukubwa wa timu hizi, lakini sina presha yoyote tumejiandaa vyema na tunaendelea kujiandaa kuhakikisha tunapata ushindi na kuelekea kwenye fainali," alisema Eymael.

Alisema kuwa lengo lao ni kuhakikisha wanapata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa baada ya kuukosa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu.

"Nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa kombe la Shirikisho Afrika ipo kwenye michuano hii ya FA na tumebakisha michezo miwili tu ambayo kama tutafanikiwa kushinda tayari tutakuwa na tiketi hiyo mkononi, huu ndio umuhimu wa mchezo dhidi ya Simba na ule wa fainali kama tutafanikiwa," alisema Eymael.

Yanga wanatarajia kurejea jijini Dar es Salaam kesho baada ya jana kucheza mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar kwenye uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

## Mlandege yatamba kushinda mechi zote

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

KOCHA wa timu ya Mlandege, Abdulhamid Rashid amesema wachezaji wake wamejiandaa kushinda michezo yote saba iliyobaki kwenye Ligi Kuu ya Zanzibar, ili kubeba ubingwa kwa kishindo kikubwa.

Mlandege iliendelea kufanya vizuri katika ligi hiyo na kubaki kileleni mwa msimamo baada ya juzi kupata ushindi wa 1-0 dhidi ya maafande wa JKU.

Bao hilo pekee la Mlandege lilifungwa na Yahya Haji katika dakika ya 72 baada ya kupiga shuti kali na kujaa langoni mwa JKU.


Akizungumza baada ya mchezo huo, Abdulhamid alisema kwa sasa timu hiyo imetilia mkazo michezo yake hiyo, ili kuhakikisha wachezaji wanacheza kwa hamasa kubwa zaidi lengo likiwa ni kubeba ubingwa wa Zanzibar kwa msimu huu wa 2019/2020.

Aidha, kocha huyo alizungumzia mchezo wake wa leo Mafunzo na kusema wamejiandaa kuhakikisha wanatoka na ushindi mnono ili kuendelea kuwapa raha mashabiki wake.

Alisema kuwa hadi sasa hana wachezaji majeruhi, hivyo kikosi chote kitashuka dimbani dhidi ya mchezo huo kikiwa fiti.

Michezo
Alhamisi Julai 9, 2020
Nipashe

HABARI UK 22



## De Gea anaweza kucheza miaka 10 zaidi – Schmeichel




Wachezaji wa Simba na viongozi wakishangilia ubingwa na kombe lao wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya mechi dhidi ya Namungo FC, jana. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# SIMBA HESHIMA

●●●Yakataa sherehe za ubingwa wao kuwekwa doa kama ilivyokuwa msimu uliopita, Morrison ang'aa Yanga ikiipiga Kagera ...

**Na Somoe Ng'itu, RUANGWA, Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa 2019/20, Simba ya jijini Dar es Salaam, wameendelea kuupa heshima ubingwa wao baada ya kutoka suluhu na Namungo FC katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa mkoani Lindi jana.

Sare hiyo imeifanya Simba ambayo iliwapumzisha nyota wake mbalimbali wa kikosi cha kwanza ifikishe pointi 81 huku Namungo yenyewe iweke kibindoni pointi 60 na kuendelea na kampeni ya kumaliza kwenye nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Simba wamekabidhiwa kombe la ubingwa wa msimu 2019/20 pamoja na medali na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamisi Kigwangwala ambaye aliongozana na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania ( TFF), Wallace Karia na wadhamini wakuu, Vodacom.

Abeid Athumani wa Namungo aliteuliwa kuwa mchezaji bora wa mechi hiyo ya jana na kupata zawadi ya Sh.500, 000 kutoka katika benki ya KCB, ambao ni mmoja wa wadhamini wa ligi hiyo.

Licha ya Simba kupata sare ya tatu mfululizo, inamaliza msimu huu ikivuna pointi nne kutoka kwa Namungo baada ya kupata ushindi wa mabao 3-2, katika mchezo wa kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam.

Wenyeji Namungo walianza kwa kasi mchezo huo lakini golikipa wa Simba, Beno Kakolanya aliwahi kupangua shuti kali iliyopigwa na mshambuliaji, Steve Nzigamagabo dakika ya pili na kuwanyima bao la mapema.

Namungo waliendelea kulishambulia lango la Simba kupitia kwa Hashim Manyanya lakini Kakolanya kwa mara nyingine alipangua shambulizi hilo na Meddie Kagere akauondoa mpira jirani na goli lao dakika ya tisa.

Simba ilijibu shambulio hilo kupitia kwa Kagere lakini golikipa wa Namungo, Nurdin Balora, aliwahi kupangua shuti la Mnyarwanda huyo aliyekuwa katika nafasi nzuri ya kufunga dakika ya 10 huku dakika ya 17 Kagere akapiga pembeni baada ya kuuwahi mpira kutoka kwa Khamisi Khalifa wa Namungo.

Dakika ya 18 Mbrazil, Tairon Santos aliwahi kutoa nje mpira uliopigwa na Abeid Athumani wa Namungo na kuwanyima tena wenyeji nafasi ya kufunga huku Simba ikipoteza nafasi ya kufunga baada ya mpira wa kichwa uliopigwa na Yusuph Mlipili kutoka nje dakika ya 26.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi ile ile lakini Lucas Kikoti aliinyima timu yake bao baada ya mpira wa kwanza wa faulo uliopigwa dakika ya 53 kuishia mikononi kwa Kakolanya huku faulo ya pili dakika moja baadaye ikipaa langoni na kutoka nje.

Dakika ya 61 Kikoti tena alipiga nje akiwa jirani na Kakolanya wakati mabeki wa Simba wameshapotea na kupoteza nafasi ya kupata bao la kuongoza huku Balora akidaka krosi ya Ajibu, lakini Namungo wataiwaza nafasi aliyoipoteza Kikoti baada ya Kakoanya kuokoa mpira wakiwa wamebaki wawili dakika ya 64.

Kagere akiunganisha pasi fupi ya Deo Kanda, alikosa bao baada ya Balora kudaka shuti hilo dakika ya 88 huku sekunde chache shuti la Athumani wa Namungo likigonga mwamba na kurudi uwanjani.

**Namungo;** Nurdina Balora, Minza Christoms, Edward Charles, Steven Dua, Carlos Protas, Hamisi Khalifa, Hashim Manyanya/ Jamal Issa (dk 72),Steve Nzigamagabo, Bigirimana Blaise/ Jovin Kelvin (dk 29), Lucas Kikoti na Abedi Athumani.

**Simba;** Beno Kakolanya, Haruna Shamte/ Hassan Dilunga ( dk 64), Mohammed Hussein/ Shiza Kichuya (dk 73), Tairon Santos/ Gadiel Michael ( dk 51), Said Ndemla, Miraji Athumani ''Sheva', Muzamiru Yassin, Meddie Kagere, Ibrahim Ajib/ Cyprian Kipenye ( dk 72), na Francis Kahata/ Deo Kanda ( dk 64).

**Wakati huo huo,** Yanga jana iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezea mjini Bukoba.

Kosa lililofanywa na beki wa Kagera Sugar, Erick Kyaruzi la kuukosa mpira na kupiga hewa, ukamkuta Benard Morrison akiwa kwenye wingi ya kulia, alimchambua kipa Benedict Tinoco na mpira kujaa wavuni kwenye dakika ya 78.

Ilikuwa ni sekunde chache tu baada ya Morrison huyo huyo kupiga shuti kali lililoonekana kwenda wavuni, lakini kipa Tinoco alipangua.

Nafasi ambazo Kagera Sugar watajutia zaidi ni dakika ya 35, Kelvin Sabato alipopiga shuti lililookolewa kwa ustadi na kipa Farouk Shikalo, huku dakika ya 62, Shikalo akiokoa kwa mguu krosi iliyounganishwa na Abdallah Seseme.

## Vodacom yaipongeza Simba kutwaa ubingwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi Vodacom Tanzania, ambayo ni mdhamini mkuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara wameipongeza timu ya Simba kwa kutwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu huu 2019/2020. Pia kampuni hiyo imezipongeza timu zote zilizoshiriki VPL msimu huu.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara wa Vodacom, Linda Riwa, alisema mpira wa miguu ni mchezo pendwa na muhimu sana hapa nchini na duniani kote.

"Tunajivunia sana kuwa sehemu ya Ligi Kuu ya Tanzania Bara, kwani inaendelea kukua na kuboreshwa mwaka hadi mwaka. Pongezi zetu pia ziwaendee viongozi wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Bodi ya Ligi, klabu zote shiriki, waandishi wa habari, wadhamini wenza pamoja na Watanzania wote kwa ujumla kwa kushiriki kikamilifu katika Ligi Kuu mwaka huu," alisema Riwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >